# Kitabu cha vitendo juu ya ulinzi wa mtoto



**Kulindwa, kupendwa, kuthaminiwa**

# Utangulizi wa kitabu kazi

*Umoja ni nguvu!*

Hiki **Kitabu kazi cha Ulinzi wa Mtoto** kimeandaliwa kutoka kwenye vyanzo na uzoefu mbalimbali wa mafunzo kwa vitendo.

Kimelenga kumwezesha mtu yeyote anaye fanya kazi kwenye rasilimali duni au maeneo ya kitamaduni ambapo hakuna muundo imara wa kitaifa wa ulinzi wa mtoto.

**Kwa nini ulinzi wa mtoto ni muhimu? Ni muhimu kwa sababu:**

- Watoto walio lelewa kwenye mazingira ya afya na rafiki wana uwezekano zaidi wa kuwa na matokeo mazuri ya Maisha: kwenye afya ya kimwili, kiakili, kimasomo, kwenye tabia zao na maendeleo ya kijamii.

- Watoto walio fanyiwa unyanyasaji au kutokujaliwa mara nyingi wana matokeo mabaya kijamii, kitabia na kiafya wawapo wadogo au hapo baadae kwenye maisha yao.

- Mtoto wa asili yeyote wa umri, jinsia, taifa, dini na hali yoyote ya kiuchumi na kijamii anaweza kuwa muhanga wa kutokujaliwa na unyanyasaji wa mtoto. Hii ina maanisha inatuathiri sote.

- Sote tunataka kuzuia mateso ya watoto ili waishi kwenye kizazi chenye afya na kilichofanikiwa. Watoto wenye afya hutengeneza taifa lenye afya. Kila kizazi ni tumaini la baadaye.

## Maana za kisheria

Mtoto anaelezwa kama mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Kuna sheria nyingi za kimataifa ambazo zina onyesha haki za watoto na zinaleta picha chanya ya kinachoweza au ambacho kinatakiwa kufanyika kuwalinda watoto. Kwa mfano, Mkataba wa Umoja wa mataifa juu ya haki za mtoto unaeleza vile watoto wana haki ya kuishi, afya, elimu na sauti zao kusikika. Lakini tunafahamu ukweli ni kwamba watoto wengi wanateseka na hakuna msaada wa vitendo unaopatikana. Kwenye hali ya kufikirika kuna polisi wa kutosha, watendakazi jamii, mahakama rafiki za watoto na msaada wa kisheria usio wa malipo ili haki ifanyika. Lakini tunafahamu kuwa hatuishi kwenye hali ya kufikirika. Kwa hiyo, watoto wanaendelea kuwa kwenye hatari ya unyanyaswaji na kudhuriwa na kwa wale wanaojali kuhusu hili, inakuwa ni hali isiyo na msaada wala matumaini.

**Tumaini na vitendo**

Kitabu kazi hiki kimeandikwa ili kutoa matumaini na msaada kwa pamoja! Unategemewa **wewe**, kama mtu mzima na mtu unayejali vya kutosha kufanya mabadiliko. Matatizo yaliyo mbele yetu yanaweza kuleta changamoto. Kufanya mabadiliko kunahitaji juhudi, matendo ya kudhamiria na shahuku ya kufanya maamuzi sahihi kwenye hali mtu anazoweza kujikuta ameingia.

.

*Kwa kawaida hakuna jibu moja kwa matatizo yenye utata/mkanganyiko!* Mafunzo yameundwa kuzingatia hali halisi ya maisha na kupata suluhisho bora kwa tatizo husika katika mazingira halisi. Kimeandikwa ili kutoa kanuni na hatua za vitendo ambazo zitaongeza uelewa na kuibua mjadala na natumaini itapunguza hatari kwa watoto.

**Msaada wa Mungu**

Kama wakristo hatujaachwa peke yetu kuhangaika gizani (Yohana 8:12). Biblia inatusaidia kufanya maamuzi yetu yasimamie kwenye maadili ambayo yatatuongoza. Zaidi, tunayo nguvu na ujasiri ambao Mungu hutupa kupitia Roho Mtakatifu, ambaye hutufundisha, hutuongoza na kutuonyesha kwenye kweli yote (Yohana 14: 15-27). Pia hutupatia amani kwa mioyo yetu yenye masumbuko.



## Miongozo ya wakufunzi na wawezeshaji 

### Mafunzo kwa muktadha rahisi na wa kijijini

Tafadhali kumbuka huhitaji dhana maalum au pesa nyingi ili kufundisha vizuri. Wala huhitaji kuwasilisha kwa njia ya mawasilisho ya power point ama umeme. Yesu alifundisha kwa kutumia mifano rahisi kutoka kwenye maisha au mazingira asili ambayo yalikuwa yakimzunguka. Kwa mfano: 'angalia ndege wa angani..' au 'mpanzi alikwenda kupanda..' Hivyo tafadhali angalia fursa ulizo nazo na sio changamoto za ambavyo hauna.

Wakati unapo panga au kujiandaa kufanya mafunzo ya usalama na ulinzi wa mtoto kwenye maeneo ya vijijini au mazingira ya kitamaduni, tafadhali zingatia mawazo haya:



Africans at Home.

- Usiwachukulie watu ambao hawana elimu kama vile hawaelewi mambo
- Kila mtu anaweza kutoa maarifa na uzoefu wa maisha
- Usiwashushe wala kuwadharau watu, onyesha heshima
- Angalia maadili na kanuni za tamaduni ya wale unao zungumza nao.
- Zungumza lugha yao (yenye kueleweka kwao) ….. tumia misemo ya wenyeji na mifano ya vitendo.
- Jali/ zingatia viongozi- usiwafanye kama sio wa muhimu/ kutowahusisha; waonyeshe heshima na uwahusishe
- Wakina nani ni washawisi? wahusishe
- Usiaibishe watu; usiwafanye watu au mila kuonekana mbaya
- Zingatia kwenye jamii, baraka za vizazi na mshikamano wa familia
- Kila mmoja anataka kulijenga taifa lake- watoto ni sehemu ya hili
- Maarifa mjumuiko- watu hufanya maamuzi kwa makubaliano
- Amini kuwa watu wanaweza kung'amua matatizo yao wenyewe – mara nyingi wanaweza kuwa na ufumbuzi wao wenyewe.

## KANUNI ZA JUMLA ZA UFUNDISHAJI[2]

1.Jiandae vizuri. Usifikiri utafundisha kwa ufanisi kwa kusoma mwongozo tu.
2.Omba unapokuwa ukijiandaa: jiulize, 'fundisho hili linaugusaje moyo wangu mwenyewe?'
3.Tumia mifano ya wewe mwenyewe kama inahusiana kwenye kuelezea jambo
4.Hamasisha wasikilizaji wako washiriki; uliza maswali na himiza maswali
5.Tumia viungo vyako vyote kufundisha kwa shauku na nguvu!
6.Andaa somo kuendana na muda uliopewa. Usiharakishe kwenye uwasilishaji- fanya somo liwe fupi kama ni lazima na utamalizia sehemu iliyobaki wakati mwingine
7.Jisikie huru tu kutumia somo moja kama la pekee ikiwa ndilo ulilopata muda kufundisha.
8. Kumbuka kwamba hili ni jukumu takatifu na Mungu yuko upande wako!




**Andalio la somo:**

Kila somo:

- linaweza fupishwa au kurefushwa kulingana na **muda** ulionao
- Lina **lengo** kuu hivyo unaweza kuongozwa kwenye ujumbe mkuu.
- Lina '**kivutio**' au kiburudisho ili kupata umakini na ubunifu wa kundi. Kama una mfano tofauti kulingana na lengo kuu, tafadhali tumia.
- lina **mawazo muhimu**, ambayo ni muhtasari wa maudhui
- Lina maliza kwa **maombi**. Unaweza kuyasoma maombi tu au kuomba kwa maombi yako mwenyewe.

**Funguo za alama:**

Mwezeshaji anafundisha mbele ya darasa na kila mmoja akisikiliza



Tafakari binafsi darasani



Vikundi vidogo vidogo vya watu 3-5



kundi kubwa kutoa Mawazo na majibu

 kutafakari

## Somo la kwanza: Biblia inatuambia nini kuhusu watoto?

(Vifaa: karatasi na penseli kwa kila mtu)

**Lengo:** kuwapa walimu na wawezeshaji uelewa wa msingi juu ya Biblia inachosema kwetu kuhusu watoto na kuhusu ulinzi wa mtoto.

**Kivutio:** Inua Biblia. Halafu inua juu karatasi yenye umbo la moyo. Weka moyo ndani ya Biblia. Kama tukiangalia ndani ya Biblia tutaona moyo wa Mungu kwa watoto.



**Mawazo muhimu:** Biblia imejaa njia nyingi halisi za kuishi. Kabla hatujaelewa vizuri ulinzi wa mtoto, lazima tuuelewe moyo wa Mungu kwa watoto. Kwa hili, tutaangalia sehemu mbili: Biblia na sisi wenyewe.

### Fundisho kuu

Ninakwenda kukupa dakika moja utafakari. Fikiria kuhusu watoto walio kwenye Maisha yako. Ni wakina nani? Watoto wako, au Ndugu zako, majirani zako, ni watoto wa kanisani kwako? Unajisikiaje kuhusu wao?

*PUMZIKA kwa dakika moja*

Sote tunawajali watoto walio kwenye Maisha yetu, na tunawatakia wema.

**Kazi binafsi:** Muda: dakika 10

*Mpatie kila mmoja karatasi na penseli*

Chora mchoro wa mtoto katikati ya karatasi na mzungushie mtoto mambo yanayo onyesha dunia salama na yenye upendo kwa watoto. ( kwa mfano, nyumba, miti, familiya, shule, bustani, kanisa na kadhalika…)

Muonyeshe jirani yako picha yako.: mwambie jirani yako picha yako ina maanisha nini na inawakilisha nini kuhusu moyo wako kwa watoto.

**Kundi kuu:**



Nani angependa kulionyesha kundi picha yake? 😊

Picha uliyo chora kwa namna inajumuisha mawazo ya furaha, ulinzi, chakula, mchezo, kanisa, shule – mambo ambayo ungempatia kila mtoto kama ungeweza.

Unaweza ukawa hujagundua, lakini picha yako inaonyesha moyo wa Mungu kwa watoto. Yesu anasema kwamba hata kama tunawajali watoto sana na tunataka kuwapa vitu vingi vya kustaajabisha, Mungu anawajali zaidi ya ambavyo sisi tunawajali:

Sikiliza hii kutoka Luka 11: 11-13

“maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimuomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai atampa ng’e? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba yenu aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamombao?”

Mistari inatuonyesha kwamba Mungu ni Baba mwema, ana nia mazuri kwa watoto na sio kuwadhuru.



K**azi ya kundi dogo:** dakika 15

Hebu tufikiri ni nini kingine Biblia inasema kuhusu watoto. Angalia mistari hii na utengeneze orodha ya mawazo ya kibiblia kuhusu watoto na moyo wa Mungu kwao. Ndani ya makundi yenu kila kundi liangalie mstari ( lipatie kila kundi mistari michache)

*Mathayo 18:6*

*Yeremia 1:5*

*Zaburi 139:13-16*

*2 Timotheo 3:14-15*

*Mathayo 18:10*

*Mathayo 19:13-14*

*Mathayo 18:1-5*

*Marko 9:35-37*

*Mathayo 21:15-16*

*Zaburi 127:3-5*

 **Mrejesho  kutoka kwenye kazi za kundi (hapa ni mifano ya majibu)**

Mstari wako unasema nini kuhusu Mungu?

*“Bali atakaye mkosesha mmoja wa wadogo hawa waniaminio yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari”*

*Mathayo 18:6*

<u>Biblia inasema  watoto ni wa thamani kwa Mungu, yeye ni mlinzi wao na atawa hukumu wale wanao wadhuru.</u>

*Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua,” Yeremia 1:5*

*Maana wewe ndiwe uliye niumba mtima wangu, Uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana, mifupa yangu haikusitirika kwako, Nilipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi kwa pande za chini za nchi; Macho yako yaliniona kabla sijakamilika’ chuoni mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizo amriwa kabla hazijawa bado.*

*Zaburi 139: 13-16•*

<u>Mungu alimuumba na anamjua kila mtoto toka ndani ya tumbo la mamaye.</u>

*Bali wewe ukae katika mambo yale uliyo fundishwa na kuhakikishwa, kwa mama unajua ni akina nani ulijifunza kwa; nay a kuwa tangu utoto umeyajua maandio matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa Imani iliyo katoka Kristo Yesu. 2 Timotheo 3:14-15 •*

*Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 18:10*

<u>Watoto wana Malaika wao wakiwaangalia</u>

*Ndipo akaletewa watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea; wanafunzi wake wakawakemea. Lakini Yesu akasema, waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao. Mathayo 19: 13-14*

<u>Mungu anawalinda watoto na anawakaribisha kwa upendo</u>


*“Saa ile wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akamwita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, akasema, Amini, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni” Mathayo 18:1-5*

*“Akaketi chini, akawaita wale Thenashara akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote. Akatwaa mtoto, akamweka katikati yao, akamkumbatia, akawaambia, Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu, anipokea mimi, na mtu akinipokea mimi, humpokea, si mimi, bali yeye aliyenituma.” Marko 9:35-37*

*“Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona maajabu aliyoyafanya, na watoto walipopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! Walikasirika, wakamwambia, wasikia hawa wasemavyo? Yesu akawaambia, Naam; hamkupata kusoma, kwa vinywa vya watoto wacanga na wanyonyao umekamilisha sifa?” Mathayo 21: 15-16•*

*“Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, uzao wat umbo ni thawabu. Kama mishale mkononi mwa shujaa, Ndivyo walivyo wana wa ujanani. Heri mtu yule aliyelijaza podo lake hivyo. Naam, hawataona aibu wanaposema na adui langoni.” Zaburi 127 : 3-5.*

Mungu hutoa watoto kama zawadi, n a ni baraka, na sio mzigo wala sio kitu cha kukitumia na kukinyonya.

**Hitimisho:** 

Tunaposoma mistari hii na mingine kwenye Biblia, tunaanza kuona kuwa watoto wana wanajaliwa kwa kiwango cha juu kwenye ufale wa Mungu, na Mungu ana maanisha huhusu kuwatunza. Hahitaji kuona mtoto ana teseka kwenye mikono ya rushwa au unyanyasaji, na hatoacha uovu utendeke juu ya watoto. Kwa kustaajabisha, Mungu anatutaka sisi kusaidia kulinda na kujali watoto wake wa thamani.

***Funga kwa maombi:*** *Baba, asante kwa kuwa unawapenda na kuwalinda watoto na umetuita sisi pia kufanya hivyo. Tafadhali tusamehe kwa kushindwa kushika nafasi zetu kwenye kuwajali watoto. Tusaidie kwenye mafundisho yetu tujifunze namna nzuri ya kuwa sauti zao. Katika jina la Yesu. Amina.*

## **Somo la pili: Utoto**

(Vifaa: asali na limao)

Lengo: kuelewa jinsi watoto wanavyojifunza na kukua na kutafakari mitazamo yetu wenyewe kwa watoto.

Mawazo muhimu: tunahitaji kufahamu kile watoto wanahitaji na kutambua njia ambazo zinaweza kuwa zinarudia mifumo mibaya ya utoto wetu wenyewe

Kivutio: tupige kura: Je, ni rahisi kuwa mtoto? Onyeshe mkono. Nani anasema rahisi? Nani anasema vigumu?




### **Fundisho kuu**

Je utoto wako ulikuwaje?

Mambo ya kufurahisha? Kama asali?

Mambo ya kuhuzinisha? Kama limao

Labda ulifanya uamuzi huo kulingana na uzoefu wako mwenyewe. Fikiria juu ya utoto wako mwenyewe. Sote tuna kumbukumbu nzuri tamu za kukua. Na pengine sisi sote tuna kumbukumbu ambazo hazina furaha. (waonyeshe asali na limao). Wacha tutumie dakika chache kufikiria juu ya kumbukumbu ya furaha- labda wakati ulihisi salama au kupendwa, labda mwalimu maalum ambaye alikutia moyo. (Dakika 2)

Sasa fikiria juu ya kumbukumbu ngumu- labda ulitendewa vibaya na mzazi wako au jamaa wengine. Labda uliona aibu au hofu shuleni. Labda ulikuwa na njaa sana. (Dakika 2)

Tafadhali shiriki na mtu mwingine moja ya kumbukumbu zako.

Maoni kwa kikundi kikuu? Kutoka kwa kundi zima hebu tusikie kutoka kwa watu wawili: mmoja wa furaha na kumbukumbu moja mbaya (ikiwa watu wanafurahi kushiriki).

Hapa kuna swali lingine: ikiwa una uzoefu mbaya kwa mfano kwamba ulipigwa kwa ukali ukiwa mtoto, je, hiyo imekufanya utake kuwa sawa au tofauti na watoto wako mwenyewe?

Kwa nini tulifanya zoezi hilo? Ni kwa sababu tunajifunza kutokana na uzoefu wetu. Wakati fulani tunataka kufanya kinyume cha yale yaliyotupata na wakati fulani tunafanya vivyo hivyo.

<u>Kwa mfano:</u>

1.Paul alipokuwa mtoto mdogo alipolowesha kitanda na baba yake akampiga. Sasa Paul ana watoto na wakati mwanawe analowesha kitanda, Paul anajaribiwa kumpiga lakini anakumbuka jinsi alivyokuwa na hofu na huzuni, hivyo anajaribu kuwa mpole. Paulo anajaribu kuwa tofauti.

2. Mary alipokuwa shule ya msingi, walimu walimcheka alipopata jibu kimakosa. Ilimfanya akose furaha na aibu. Sasa Mary ni mwalimu na anawacheka wanafunzi wanapofanya makosa. Mary anarudia jambo lile lile alilopitia.

**Swali: Vipi kuhusu wewe?** Unapofikiria kuhusu kumbukumbu za asali na ndimu… ni aina gani za mambo ya furaha unarudia ukiwa na watoto sasa? Je, unarudia mambo gani magumu?

*Ombi: Bwana, mara nyingi tumefanyiwa vibaya na tumeumizwa na watu wakubwa hata wazaia wetur. Utuponye ili tuweze kuhua uzima na amani. Amina*

Imba wimbo kabla ya kuendelea.

**<u>Tufikiri hili: mtoto ni nani?</u>**

Mwenye wazo lolote? Ina maanisha nini kuwa mtoto. Maana ya mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18.

Kwa nini watoto wanahitaji kulindwa zaidi ya watu wazima? ( kwa sababu ni wadogo, hawajakua kiakili, ni tegemezi). Lakini watoto wote ni sawa? Je, mtoto wa miaka mitano yuko saw ana wa miaka 10? Au wa miaka kumi na tano? (Hapana)

Chora mstari kutoka 0------------------18.

Kuwa mtoto ni maendeleo ya muda mrefu! Kumbuka mtoto ni mtu anaye badilika na kukuwa mara kwa mara.

*For example: Kwa mfano:*

Mtoto mchanga ana mahitaji mengi kama vile (mifano?) …maziwa, joto, kufanywa wajisikie vizuri (huru), kuoshwa, mahusiano kutoka kwa mama. Bila haya mtoto hawezi kukua kimwili au kihisia. Kumbuka kuwa watoto wanajifunza kwa kuangalia na kujua kuwa wako salama.

Kwenye umri wa mwaka mmoja, mtoto ana tambaa au kutembea. Hatari ni zipi sasa? ( ajari, moto, kukabwa na vitu)

Vipi kuhusu miaka 6? ( anakuwa anaweza kujitegemea zaidi, anawaamini kwa urahisi watu asio wafahamu ambao wanaweza kutaka kumnyanyasa)

Je, miaka 13 ? labda mitandao, labda mahusiano ya kingono ambayo ni hatari, kufuatilia mambo ya ngono kwa sababu ni wadadisi.

Toa mifano ya namna wanahitaji kulindwa kwenye hatua tofauti tofauti za Maisha yao. Kwa mfano:

Mtoto mchanga hawezi kukimbia wala kujiingiza kwenye madawa ya kulevya. Lakini mtoto mchanga anaweza kuumia kirahisi kama atadondoshwa au kutikiswa.

Mtoto wa miaka saba anaweza kudanganywa na kumfuata mtu. Lakini pia anaweza kujifunza kuepuka hatari.

Mtoto wa miaka kumi na mbili anaweza kushawishika kuangalia video za picha ngono.

Any other ideas? Mawazo mengine zaidi?


## Somo la tatu: Ulinzi wa mtoto ni nini?

(vifaa: karatasi kubwa chache na kalamu za kuchorea au rangi)

**Lengo:** kutusaidia kufikiri kuhusu ukweli kwamba tunalinda na kujali vitu tunavyo vithamini.

**Kivutio:** kama nikiwa natembea pembeni mwa barabara na kutambua kuwa nimedondosha kipande cha karatasi chakavu ambacho nilikuwa nacho mfukoni mwangu, Je, nitaanza kukikimbilia? (labda hapana) Vipi kama nikidondosha simu yangu? (Ndio) kuna utofauti gani? Tunalinda vitu tunavyo vijali.

**Mawazo muhimu:** watoto wanahitaji kulindwa ili wasidhurike kwenye hatua mbalimbali za maisha yao.

**Fundisho kuu** 

1. Unaulindaji mwili wako usipate maambukizi wala kuumia? Kwanza kabisa, tambua hatari.

Kwa mfano- hizi ni hatari zilizo kwenye Maisha yetu ambazo kikawaida tuna jiepusha nazo

**malaria**: unaweza kutumia chandarua, au mapazia milangoni, au kujifunika usiku

**kujikata mguu kwenye kipande cha chupa:** vaa viatu, safisha vipande vya chupa na vitu vyenye ncha kali.

**kupata ugonjwa wa ngozi**: oga, tumia sabuni

**maumivu ya meno**: piga mswaki, epuka kutumia sukari nyingi, muone daktari wa meno

**kugongwa na gari au pikipiki:** vuka barabara kwa usalama

**kutapika na kuharisha:** chemsha au chuja maji, osha matunda pika vyakula vizuri

2. Vipi kuhusu unavyolinda mali zako? Kwa mara nyingine, tambua hatari.

**Nani ana simu?** Huwa unaiacha tu popote? Hapana! Huwa unakuwa makini nayo.

**Vipi kuhusu mkoba au pochi yako?** unafahamu ulipo!

**kama una nyumba au chumba,** una ufungua, labda hata umejenga ukuta na kuweka geti.

3. Kwa nini unajali vitu vyako? Kwa sababu vina thamani sana kwako.

Angalia tena ile picha uliyo itengeneza kwenye kipindi kilichopita- kuna mtoto katikati.

Kumuweka mtoto katikati na kumjali ndio mwanzo wa ulinzi wa mtoto. Kabla hatujafanikiwa kuanza kuwalinda watoto, lazima tuwe na picha halisi ya tunawalinda dhidi ya nini. Hukuchora vitu hatari au vya kudhuru kwenye picha yako kwa sababu ndani ya moyo wako unatambua kwamba watoto hawapaswi kuishi kwa namna hiyo. Hii inaendelea kuonyesha moyo wa Mungu kwa watoto.

Hatimaye, ulinzi wa mtoto ndicho kinachotokea pale tunapo uelewa moyo wa Mungu kwa watoto.



(toa dakika 15 kwenye vikundi vidogo vidogo vijadili)

**Fikiri kuhusu ulinzi wa mtoto.** Ni zipi baadhi ya hatari na athari ambazo tunawalinda watoto dhidi yazo? Fikiri kuhusu hatari zote, kwa mfano, za kimwili, kiakili, kiroho, kijinsia



**Mrejesho wa kundi:** Unafikiri ni zipi hatari kwa watoto?

(toa mifano hapo chini kuongezea kwenye kundi)

<u>Ajari:</u> kuunguzwa na maji ya moto, Mafuta, maziwa, uji- kugongwa na gari au pikipiki- kuanguka kwenye simu au kwenye nje ya jengo- kushituliwa na umeme- kukabwa na kitu- kukatwa au kuumizwa na kipande cha chupa au mashine

<u>Vishawishi vibaya</u>- watoto wengine, watoto wakubwa wengine (vijana), picha za video, mitandao,madawa ya kulevya, pombe

<u>Unyanyasaji na unyonyaji</u>- kupigwa, kubakwa, kufanyishwa kazi kupita kiwango na kudanganywa



Kumbuka! Watoto wenye ulemavu wana mahitaji zaidi na kwa wengi wao hawatakua kimwili na kiakili sawa na umri wao.




**!** Kazi za kufurahisha! Fanyeni kazi kwa pamoja kwenye makundi muandae **mabango ya kikundi chenu wenyewe kwa ajili ya ulinzi wa mtoto. Muwe wabunifu!**

*Kwa mfano:*

*‘Safe and happy children protected by adults’*
*‘Watoto walio salama na wenye furaha hulindwa na watu wazima’*

*Children in a circle of safety! Watoto kwenye mduara wa usalama!*

 **Kila mmoja atazame bango la mwenzake!**

*. Tunaweza kufikiri mambo mengi ambayo watoto wanaweza kulindwa dhidi yake, lakini zaidi ya yote* ***ulinzi wa mtoto*** *ni jitihada za kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za unyanyasaji.*

Soma Mithali 31: 8-9:

*“Fumbua kinywa chako kwa ajil]i yake bubu; uwatetee watu wote walio achwa peke yao; Fumbua kinywa chako, uhukumu kwa haki; uwapatie maskini na wahitaji haki yao”*

Kama sisi ni wazazi au walimu, mashangazi au wajomba, wachungaji au wazee, lazima tufanye kila liwezekanalo kuwalinda watoto dhidi ya uovu. Mungu amemuweka kila mmoja wetu kwenye nafasi ya mamlaka juu ya watoto, n ani lazima tuwe mawakili wema kwa mamlaka zetu. Matumizi mabaya ya mamlaka juu ya watoto ni mwanzo wa unyanyasaji wa watoto.
Pale unyanyasaji wa mtoto unapotokea, **ulinzi wa mtoto** ni jibu sahihi kwa unyanyasaji. Matukio ya unyanyasaji lazima yashughulikiwe vizuri ili watoto wapata msaada unaohitajika kupona.

Soma Zaburi 82:3 -4:

*“Mfanyieni hukumu maskini na yatima; mtendeeni haki aliyeonewa na fukara; Mwokoeni maskini na mhitaji; Mwopoeni mikononi mwa wadhalimu”*

***Maombi ya kufunga****: Baba, asante kwa moyo wako wa haki kwa watoto. Unawapigania walio onewa, unawainua walio tupwa chini, unawatia moyo walio vunjika mioyo. Tusaidie kusimama kwenye nafasi wazi za watoto na kuwasemea. Tunaomba utupe nguvu. Amina*

## Somo la nne: Watoto na mahitaji yao


(vifaa: gunzi la muhindi au embe, au kitu chenye mbegu, mabango ya kugeuza ya kufundishia au karatasi)

**Lengo**:Kutambua mahitaji maalum waliyo nayo watoto na wajibu wetu wakuwalea kwenye jamii yetu ili wawe baraka.

**Kivutio**: Leta gunzi la muhindi au embe. Uliza: kuna mbegu ngapi kwenye embe? (moja). Kuna maembe mangapi kwenye mbegu (mamia). Hii inaonyesha uwezo/ thamani gani iko ndani ya mtoto mmoja.



**Mawazo muhimu**: watoto ni baraka na urithi. Zaburi 127: 3-5

**Fundisho kuu** 


Mungu ameutengeneza ulimwengu kwa ajili ya watoto kuzaliwa kama vichanga. Ametupatia watoto kwenye jamii zetu na familia zetu. Watoto wamezaliwa wakiwa wategemezi kwa walezi wao kuwalea na kuwalinda. Tukitengeneza mazingira salama kwa watoto watakuwa wakiwa salama na watakuwa raia enye tija ambao ni baraka ulimwenguni. Kumbuka tulipo zungumza kuhusu madaraka. Walio dhaifu ndio wako kwenye hatari zaidi ya unyonyaji. Watoto walemavu na viziwi wako kwenye hatari zaidi ya kunyanyaswa.

Watoto wa Afrika

- Tafakari kuhusu maembe na kama ukienda sokoni na ukanunua maembe 10 ila unaporudi nyumbani na kugundua moja limeharibika, utafanya nini? (utalitupa hilo lililo haribika ili lisiharibu na mengine). Tunataka kuwekeza kwa watoto ili kuhakikisha wako salama na hatutaruhusu waharibike.
- Watoto ni urithi. Zab 127: 3-5
- Tunawekeza kwenye kizazi kipya. Watoto ndio kizazi chetu kijacho
- Unafahamu ya kwamba 50% ya Afrika iko chini ya umri wa miaka 18. Hii ina maanisha kuna nafasi/uwezo mkubwa sana kwa mabadiliko ya bara la Afrika!

**Example: Mfano:**

Elezea kuwa kuwekeza kwenye kitu kidogo kunaleta ongezeko. Unapanda mbegu, lakini ina hitaji udongo mzuri na mazingira mazuri. Mvua, jua, kulima Ina chukua muda na inahitaji uvumilivu. Huwezi kukanyanga-kanyaga tu wakati wa upandaji mbegu. Tafakari kuhusu mtoto. Katika njia hiyo hiyo, ndivyo unavyo mlea na kumlinda mtoto.

Kundi kuu: 

Ni zipi tofauti kati ya mtoto na mtu mzima? Karibisha majibu kutoka kwenye kundi.


| **Watu wazima wakoje?** | **Watoto wakoje?** |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

Ongeza majibu yako mwenyewe baadae kama hakuna mtu yeyote aliye yataja.

**Watu wazima**: ukubwa, nguvu, uwezo wa kutambua, hawaamini kwa urahisi, ufahamu zaidi, uwezo wa kufanya maamuzi yao wenyewe, wanawaza zaidi kuhusu kodi/Ankara, majukumu, mamlaka, ujasiri.

**Watoto**: wachangamfu, wanatumainia watu, wanaamini, akili zao kama sponji- wanakumbukumbu nzuri na ni wepesi kujifunza (fikiri kuhusu kujifunza lugha… nani alikufundisha kuongea Kinyarwanda/ kiarabu/ kisukuma? ……hakuna- wamejua tu tena kabla hata hawajatembea.. Watoto wana akili kama ‘saruji iliyolowa’, kila kinacho ingia …. Wanaiga wanachoona.

Onyesha na sifongo na ndoo ya maji; hivi ndivyo mtoto anavyonyonya kwani akili zake hujifunza haraka sana. Ikiwa ni maji mazuri au maji machafu- yote yanaingia.



**Mahitaji ya watoto**

Watoto wanahitaji nini- kimwili, kihisia, kijamii, kiakili?



Kila kundi libainishe mahitaji ya mtoto. Tumia mabango ya karatasi za kugeuza.

- Kiakili
- Kijamii
- Kimwili
- Kihisia/ kiroho
- Kupuuzwa/ kutelekezwa

Kila kundi lina dakika 10 za kuandika mawazo na kumuomba mwakilishi wa kundi kuwasilisha.



**Main group- ask for group feedback. Kundi kuu- omba mrejesho wa kundi.**

*Kiakili*: elimu, kuuliza maswali, kujifunza, kuwa mdadisi, kufanikiwa, kuwa na dhana za kujifunzia.

*kijamii*: wanajisikia kuwa sehemu ya jamii husika, kusikilizwa, kuchangia, kuwa na utambulisho/ cheti cha kuzaliwa, kujua urithi wao

*Kimwili*: chakula kizuri, protini, maji, kukuwa, usalama, afya, vyandarua, maji safi na salama, usafi wa mazingira, makazi, usafi

*Kihisia*: kutiwa moyo, kuthibitishwa/ kukubaliwa, kujisikia salama, kulindwa, kuabudu, kuamini.

 Tafadhali zingatia kwamba watoto walemavu na viziwi wako kwenye hatari kubwa zaidi ya kunyanyaswa. Kwa nini?

(Majibu: hawawezi kuwasiliana vizuri, wanahudumiwa na watu mbalimbali, hawawezi kuongea na kujitetea, ni rahisi kutumiwa vibaya)

**Hitimisho**: watoto wana mahitaji maalum kwenye umri tofauti tofauti wa Maisha yao. Wanategemea watu wazima ili kupata mahitaji yao ili waweze kukuwa na kustawi.

***Maombi ya kufunga**: Baba wa mbinguni. Tafadhali tusaidie kutambua watoto wanachohitaji na tuweze kuwekeza kwao ili wakue kwenye njia salama. Kwa jina la Yesu. Amina*

## Somo la tano: Mafunzo ya Biblia juu ya madaraka na matumizi mabaya ya madaraka


(vifaa: gundi ya karatasi ngumu, gundi ya karatasi nyepesi au mtandio)

**Lengo:** angalia mada hii kwa kusoma habari ya Biblia ya Amnoni na Tamari, na chunguza jinsi unyanyasaji wa kingono inavyohusianishwa na matumizi mabaya ya mamlaka.

**Kivutio:** omba mtu ajitolee. Funga mdomo wake kwa gundi ya karatasi au mtandio au nguo. Hawawezi kuzungumza. Wanong'oneze masikioni mwao ujumbe wa kupaza sauti kwa kundi: "Kimbieni haraka kuna simba anakuja kwetu!" Angalia kama wanaweza kutoa ujumbe kwa kikundi! Ni vigumu sana kuwasiliana bila kuwa na uwezo wa kuzungumza.

Leo tunazungumza kuhusu watu walio nyamazishwa au ambao wamenyamaza. (Toa gundi ya karatasi)

**Mawazo muhimu:** sote tuna mchango kwenye kutumia madaraka na mamlaka tuliyonayo kuwalinda wale wanao hitaji ulinzi.

### Fundisho kuu  

Soma 2 Samweli 13: 1-21 au muombe mtu asome

Tamari alikuwa binti mfalme. Alikuwa Tajiri na aliyependelewa, lakini Maisha yake yaliharibiwa kwa kubakwa na Amnoni kaka yake. Hakuna mtu aliye mlinda ili kuzuia isitokee au kutaka haki itendeke kwake. Unyanyasaji unaweza kutokea popote. Mara nyingi huwa ni uonevu kwa mtu dhaifu.

Madaraka ni nini? (wait for answers from the class…) (subiri majibu kutoka kwa darasa….)

Ni pale mtu au mfumo unapokuwa na mamlaka, ushawishi au udhibiti juu ya mtu dhaifu au aliye ngazi ya chini.

**Tutafakari kuhusu aina za madaraka**: wazifa, pesa, tamaduni, kabila, nafasi, tabaka, elimu.

Kwenye utamaduni wako mwenyewe kitu gani humpa mtu madaraka na ushawishi? Ni mtu wa namna gani kila mtu ana mkubali?

Tafadhali toa mifano.

(majibu yanaweza kuwa): mtu mwenye hulka nzuri, mavazi au mtindo, mwonekano, mahali pakuzaliwa, taaluma, unafahamiana na wakina nani, elimu, kabila,

Kwa mfano: kanisani kwa kina Anna, mmoja kati ya wazee ni tajiri ambaye ni mtu mkubwa na mrefu. Ni mfanyakazi wa serikali pia. Anna amegundua kuwa wazee wengine wote n ahata Mchungaji wanaonekana kumuogopa.

*Read the passage again 2 Sam 13:1-23 and in groups, look at these questions for discussion: Soma tena kifungu cha 2 Sam 13: 1-23 na kwenye makundi, angalieni maswali haya kwa ajili ya majadiliano:*

Amnoni alisema anampenda sana Tamari dada yake kiasi kwamba ilimfanya aumwe. Unafikiri nini? Ni kweli alikuwa anampenda? Upendo ni nini?

Utaelezeaje hisia za Amnoni juu ya Tamari? Kwenye mstari wa 15 kwa nini anamchukia ghafla?

Alifanyiwa ubakaji milango ikiwa imefungwa. Unafikiri watu waliokuwa nje walijua nini kinatokea?

- Kwa nini unafikiri hakuna aliye ingilia kati?
- Ni matokeo gani ya muda mfupi na mrefu kwa tamari?

**Tafakari kuhusu madaraka**. Kwenye habari hii nani alikuwa na mamlaka? Mamlaka yana matokeo gani kwa watu? Tafakari kuhusu mtu aliye na madaraka na mtu aliye chini ya maelekezo ya wenye nguvu?

**Group work: Kazi za kundi**


Kwenye habari hii kuna Amnoni, Yonadabu, watumishi, Tamari, Absalom una Daudi. Kwenye makundi tumuangalie mmoja kati ya hawa watu, na tutafakari nani ametenda dhambi na angefanya nini kuzuia jambohili lisitokee.

Lipe kila kundi jina ( amnoni, Yonadabu, watumishi, Tamari, Absalomu na Daudi)

Na uwapatie muda wa kujadiliana maswali yafuatayo:
.
Je, mtu huyu ametenda dhambi? Angeweza kufanya nini? Kwa nini hawakufanya chochote? Unaweza kufikiri mfano ambao na wewe ulifanya vivyo hivyo?



 Pokea mrejesho kutoka kwenye kundi kuu.



Eleza: Kwenye kila somo lifuatalo tutaangalia zaidi Biblia inatuambia nini kuhusu namna ya kuwalinda watoto.

***Maombi ya kufunga***. *Baba, nisaidie kutumia madaraka niliyonayo kuwainua wengine. Tafadhali utusamehe pale ambapo tunageukia mbali na wale wanao hitaji msaada wetu. Tusaidie kufuata mfano wa Yesu ambaye aliacha kila kitu kwa sababu ya kuupenda ulimwengu. Tusaidie kujinyenyekeza chini ya mkono wako wenye uweza ili uweze kutuinua juu. Amina*

## Somo la sita: unyanyasaji wa mtoto


*(vifaa: mwamba mdogo au jiwe; sarafu au pesa ya noti, chapisha matukio au yaandike kwenye kipande cha karatasi kwa ajili ya kila kundi)*

**Lengo**: kutoa muhitasari wa unyanyasaji wa mtoto na aina zake mbalimbali.

**Kivutio**: chukua jiwe na uliweke sakafuni kisha uanze kulipiga na kulisema kwa sauti ya juu. Nimefanya kitu chochote kisicho sawa? ( Hapana, kwa sabau ni kit una si mtu). Jiwe halina hisia. Lakini mtoto anaweza kuona, kusikia, kugusa na kuhisi.

***Mawazo muhimu:***

Warumi: 13v7. Wakolossai 3:12
Watu wanatenda kama watoto ni kitu chakutumika na kunyanyasa. Lakini watoto wana haki chini ya sheria. Unyanyasaji ni dhambi na kosa. Inawadhuru watoto kwa muda mrefu maishani. Mungu atamuhukumu yeyote anaye mdhuru mtoto.

**Fundisho kuu** 

Andika orodha ya vitu vyema na vizuri duniani. (miti, familia, sherehe, muziki, chakula, rangi, ndege, asili na kadhalika)

Mungu alipo umba dunia kulikuwa hakuna dhambi. Ilikuwa ya amani, nzuri na njema. Adamu na Eva walitembea bustanini bila nguo na hawakuona aibu. Mwnz 2:25. Walitembea na Mungu mchana kweupe. Walikula chochote walichotaka Mwnz 1:29 lakini waliagizwa wasile kutoka kwenye mti wa ujuzi wa mem ana mabaya Mwnz 2:16.

Tunaposoma Mwnz sura ya 3, Adamu na Eva walimsikiliza nyoka yule mdanganyifu, na hawakumsikiliza Bwana na wakala kutoka kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Hapa ndipo uovu ulipoingia duniani. Ndipo macho yao yakafunguliwa na ghafla wakaingiwa aibu na hofu. Mungu aliwafukuza kwenye bustani na wakatengwa naye 3:24.

Kuanzia hapo, mwanadamu alitengwa na Mungu.
Orodha ya mambo yote mabaya na yasiyo sawa tunayo yaona duniani.(vita, chuki, ukatili, vifo, wizi, uzinzi.. n.k).

Mungu ana upenda ulimwengu alio utengeneza. Aliandaa mpango wa kuwarudisha watu kwenye uhusiano wa upendo na yeye. Mpango wake ulikuwa kupitia mwana wake, Yesu Kristo. Warumi 5:8. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu na akaubeba mzigo wa dhambi mwilini mwake pale msalabani. Kila mtu alizaliwa kwenye dhambi na huchagua kufanya dhambi, hii humaanisha kuwa kila mtu anahitaji kusamehewa na Mung una kuokolewa kwa njia ya imani katika Kristo.

Kupitia Kristo tunaweza kurithi matumaini ya Maisha ya milele. Mbinguni hakutakuwa na maumivu wala huzuni tena, au vilio au misiba au ukatili.

Mfano: Onyesha sarafu au pesa ya noti- ina thamani ya kiasi gani? (jibu- ina eleza kwenye sarafu au noti) Je, inajalisha kama ni sarafu mpya au ya zamani? Kama ina ng'aa na ni mpya au ya zamani na iliyo chakaa? Je, thamani inabadilika? HAPANA. Thamani yetu iko kwenye utu wetu na vile tulivyo fanywa kwa picha yake. Kama mtu ni masikini au tajiri, mzuri au wa kawaida, haipunguzi thamani.

Wakati huo kama miliki ya thamani ya Mungu, tunaishi kwenye ulimwengu ulio anguka na kuvunjika. Watu wanaendelea kutenda dhambi kwa njia tofauti tofauti na moja ya njia hizo ni unyanyasaji wa watoto. Hii ndio mada yetu kwenye mfululizo huu wa mafunzo.

Kuna aina tofauti za unyanyasaji ambazo watoto wanaweza wakapitia::

- Kimwili
- Kihisia
- Kingono
- Kupuuzwa/ kutelekezwa

Wakati mwingine aina hizi za unyanyasaji huja pamoja. Hii inaitwa kufanywa muhanga wa unyanyasaji wa aina nyingi kwa pamoja. Kama mtoto anapitia unyanyasaji wa kimwili kuna uwezekano atakuwa anapitia unyanyasaji wa kihisia pia. Hata hivyo haiwezekana kumpiga mtoto bila kumsababishia maumivu kihisia au kisaikolojia.

**kazi za vikundi vidogo**

Soma visa hivi:


- Mariam ana miaka 13. Kaka yake anaporudi nyumbani kutoka shule ya bweni alianza kuja chumbani kwake kila usiku na kumsumbua, ana mshikashika mwili wake na kulala juu yake. Ana ona aibu na kujisikia mchafu. Hajui nini chakufanya. Una fikiri hii ni aina gani ya unyanyasaji?

- Felix ana miaka 8 na ana hudhuria shule yako ya Jumapili. Mama yake alifariki mwaka uliopita nab ab yake ameoa mke mwingine tena. Alikuwa ni mtoto mwenye furaha lakini hivi karibuni anaonekana kuwa mchovu na mwenye huzuni. Umegundua nguo zake zimechanika na chafu. Unapo jaribu kuzungumza naye ana ruka na kuonekana kuogopa. Una fikiri nini kitakuwa kinatokea nyumbani?

- Tabitha ana umri wa miaka 14. Ni mlemavu wa utindio wa ubongo. Hawezi kuongea wala kutembea. Ana ishi na mama yake. Mama yake anafanya kazi sokoni kila siku kuanzia asubuhi mpaka jioni. Tabitha anaachwa kwenye mkeka ndani ya nyumba, hali wala kunywa chochote mpaka mama yake anapo rudi. Unyanyasaji wa namna hii unaitwaje?

 Kundi kuu- mrejesho kutoka vikundi vidogo

**Mariam:** huu ni unyanyasaji wa kingono unaofanywa na kaka yake
**Felix**: anaonekana ametelekezwa na labda unyanyasaji wa kimwili
**Tabitha**: kutelekezwa, labda na unyanyasaji wa kihisia



Swali: Ni aina gani ya unyanyasaji unatokea kwenye jamii yako? Unaonaje ? Unafikiri hii itakuwa ina waathiri vipi watoto?


***Maombi ya kufunga**: Eh Bwana mpendwa, wahurumie hawa watoto! Tafadhali tuma msaada na ulinzi wako juu yao! Kwa jina la Yesu! Amina.*

## Somo la saba: Unyanyasaji wa kimwili

**Lengo**: kuadabishwa kote kunatakiwa kufanyike kwa lengo la kufundisha na kuongoza. Unyanyasaji wa kimwili sio tendo la upendo.

**Kivutio**: Gonga mkono kwa nguvu mkono wako juu ya meza iliyo mbele yako. Imeumiza meza? Hapana kwa sababu meza imetengenezwa kwa mbao. Fikiri kama huyu angelikuwa ni mtoto. Hicho ni kitu kizuri kufanya? (liulize kundi). Vipi kuhusu mstari huu:
Warumi 13:7 upendo haumdhuru jirani. Wagalathia 5:22,23 tunda la roho ni upole.

**Mawazo muhimu**: Watoto wanahitaji kuadabishwa, lakini wasidhuriwe, na kuadabishwa kusifanywe kwa hasira. Kuadabishwa kunatakiwa kufanywe kwa upendo na kwa ajili ya mema ya mtoto mwenyewe. Unyanyasaji wa kijinsia unasababisha kuumia, hofu na makovu ya daima.



### Fundisho kuu

Mifano ya unyanyasaji wa kimwili ni: kupigwa, kuchapwa mijeledi, kupiga mtoto kwa fimbo au silaha, kusababisha jeraha, kuadabishwa kwa ukali sana, kupiga mtoto usoni au kichwani ama mkononi, kupiga mateke au kurusha ngumi kwenye mwili wa mtoto, kuunguza, kufunga Kamba, kukaba, kusukuma kwenye maji.

Ukweli: Watoto wanahitaji kuelewa kilicho sahihi na kisicho sahihi. Ingawaje wazazi wana wajibu wakuwaadibisha watoto wao, hii haimaanishi inahitaji kujumuisha adhabu za kimwili. Kuna njia nyingi ambazo mtoto anaweza kuadabishwa kwa njia ya kujenga ambayo haimsababishii hofu na maumivu. Mtoto anapokuwa ameadhibiwa kimwili basi iwe inaendana na umri wake na umbo na isifanyike kwa hasira. Watoto wanatakiwa kujua kwamba wanajua wanapenwa na kujaliwa.

Maandiko yanasemaje?

Ebr 12:10 baba mzuri ana adabisha watoto wake kwa upendo na kwa ajili ya mema ya watoto

Efs 4:2 kuwa mnyenyekevu kabisa na mpole

Efs 6: 1-4. Watoto wanatakiwa kuwatii na kuwaheshimu wazazi wao, na wazazi wasiwakatishe tamaa watoto wao.

Kol 3:12 tunatakiwa kuvaa wema, huruma na uvumilivu.

1 Kor 13:4 upendo huvumilia na kujali.

Rum 13:10 Upendo haumdhuru jirani

**Vikundi vidogo: dakika 15. Jadili maswali haya.**

- Uliadhibiwa vipi na wazazi wako mwenyewe?
- Je, unafikiri kwamba adhabu ya kimwili ni jambo jema? Kwa nini au kwa nini?
- Biblia inaposema acha fimbo na kumharibu mtoto ina maana gani?
- Biblia inaposema katika hasira yako usitende dhambi, hii inamaanisha nini?
- Ni faida gani za kumpiga mtoto? Je, kuna hasara gani?
- Je, unajua tofauti kati ya kumpiga mtoto na kumdhulumu? Tofauti ni nini?

Fundisho kuu;

Andika neno ‘**ADHABU**’ kwenye bango. Waombe washiriki wakumbuke maneno yanayo husiana na adabu- ina maanisha nini? Eleza kwamba adabu inatokana na mzizi wa neno ‘mfuasi’ na ina maanisha kuelekeza na kufundisha ili kuzalisha sifa/ hulka fulani na tabia. Watu wengi wanakosea kufikiri kuwa kuadabisha ni adhabu tu. Kwa uhalisia kuadabisha kuna jumuisha mbinu mbalimbali ambazo husaidia kutengeneza sifa chanya na tabia kwa mtoto. ]

Moja kati ya mistari iliyo nukuliwa sana kwa namna gani tunatakiwa kuwaadabisha watoto ni Mithali 13:24, ‘yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; bali yeye ampendaye humrudi mapemaa.’ Mara kwa mara mstari huu hutumika kama kisingizio cha adhabu kali za kimwili kwa watoto.

Soma Zaburi 23:4. Je, ni ipi nafasi ya fimbo ya mchungajikwenye kifungu hiki? Fimbo yako na gongo lako vyanifariji). Mchungaji hatumii bakora (fimbo yake) kuwapiga kondoo, zaidi ya kuwaongoza na kuwarudisha kwenye njia sahihi, kwenda kwenye uelekeo sahihi na wakati mwingine kuwaokoa hatarini. Kama wazazi, walimu au walezi tunao wajibu kuwapatia watoto wetu heshima kwa mamlaka, na kuwasaidia wajifunze adabu. Kama watu wazima ni wajibu wetu kuwaongoza na kuwalinda watoto walio kwenye uangalizi wetu. Hiyo haimaanishi kuwa thibiti kwa kuwatisha kwa adhabu. Tuombe pamoja kwamba tuendelee kuelewa jinsi ya kuongoza, kulinda na kujali watoto kwa njia za kimungu.

**Hii hapa ni habari ya kweli kutoka Tanzania (kwa majina yaliyo badilishwa.**

Vedasto alikuwa akisoma shule ya msingi Mlimani. Alipelekwa kwa mwalimu mkuu kwa kuchelewa darasani kila siku wiki hii. Mwalimu mkuu alichukua fimbo na kumpiga Vedasto mara 5. Vedasto aliangukia kwenye ukuta wa tofali na akaumia kichwani na kufa. Mwalimu mkuu aliwaambia polisi ilikuwa ajari. Wazazi wa Vedasto hawakua na pesa za kupata msaada wa kisheria. Mwalimu mkuu bado yuko shuleni.



Kwenye vikundi vidogo, tumia dakika 15 na tafakari kuhusu matatizo kama matokeo ya hili?

- No justice for Vedasto and his family. Hakuna haki kwa Vedasto na familia yake.
- Other pupils may feel scared. Wanafunzi wengine wanaweza kuingiwa hofu.
- Other pupils are at risk. Wanafunzi wengine wako kwenye hatari.
- School has no way of controlling the pupils without using violence
  Shule haina namna ya kuthibiti wanafunzi bila kutumia vurugu.

Afrika, baadhi ya watoto huwa wana adhibiwa mara kwa mara mpaka inafikia kuwa unyanyasaji. Hii inaweza kutokea nyumbani. Hii inajumuisha:

Kupiga mateke, kupigwa, kuchomwa, kuzamishwa kwenye maji, kunyongwa, kupigwa kichwani na mikononi.

- Una mifano zaidi?

- Hii ina athari gani kwa watoto?

Kihisia: hofu, kutokuwa wa thamani
Kimwili: kujeruhi, maumivu, makovu, majeraha ya kichwa

**<u>Fundisho kuu</u>**

**<u>Kwa nini unafikiri watu huwa nyanyasa watoto kimwili?</u>**

<u>Majibu:</u>

Maadili ya kitamaduni**:** kufanya hivyo kwa kuwa kila mtu anafanya.

*Msongo wa mawazo: mzazi au mwalimu ana mambo mengi ya kufikiria au kufanya-hawana uvumilivu tena. Wana 'geuka' na kuvamia. Mfano:Baba Joseph amepoteza kazi yake ya kutengeneza bustani na ana wasiwasi na hajui namna gani ya kulisha familia yake. Asubuhi Joseph ana lalamika kuwa hakuna sukari kwa ajili ya chai. Baba joseph ana kasirika na ana chukua chai ya moto na kummwagia Joseph*

*Vitu vya sumu: pombe, au madawa vinamfanya mtu asielewe nini anocho kifanya. Kwa mfano: Mara nyingi mama Mariam ana kunywa pombe za kienyeji na ana lewa. Mariam anapo rudi nyumbani kutoka shule, mara nyingine mama huwa ana mrushia vitu bila hata sababu.*

*kutokujua: jinsi mtoto anaweza kudhurika kwa kupitia baadhi ya adhabu. Kwa mfano: mwalimu anatumia tawi dogo la mti kuwa thibiti watoto darasani. Wakati mwingine ana wapiga watotot usoni. Wiki iliyo pita amesababisha mtoto kuvuja damu puani.*

*Ukatili: mtu mzima kwa makusudi anataka kumfanya mtoto ateseke. Kwa mfano: Joeli ana mika tisa. Bibi yake anapokuja kukaa nyumbani, huwa natumia kipande cha mbao kumpiga kwenye vifundo vya vidole/ kiganja.*

**MADHARA WANAYOFANYWA WATOTO: mnaonaje?**

- Kuwapiga au kuwapiga watoto kunaweza kusababisha madhara kwa miili yao.
- Kuna ufahamu unaokua kwamba kutumia ukatili kuwaadhibu watoto sio msaada kwao na inaweza kuwa hatari sana hasa pale mtu mzima anapokuwa na hasira au mlevi. Kupiga watoto karibu na uso au mikono au kichwa kunaweza kusababisha uharibifu wa kudumu. Inaweza kuwa kinyume cha sheria katika nchi yako.
- Kuwapiga watoto huumiza mioyo yao.
- Kusababisha maumivu husababisha hofu.
- Watoto hawawezi kujifunza wakati wanaogopa.

**Kazi za vikundi vidogo: angalia visa hivi:**

1. Uko kwenye kikundi cha kwaya cha kanisa na mnafanya mazoezi kila ijumaa. Kuna mwanamke anaitwa Helena ambaye mara kwa mara humleta Felista, binti yake wa kambo mwenye miaka 7. Unagundua kwamba wiki chache kadhaa Felista amekatwa na ana majeraha kwenye macho yake. Nini kinaendelea kwenye mawazo yako/ ungefanya nini?

2. Kanisa lako linasimamia klabu ya Biblia wakati wa likizo ya pasaka. Kuna watoto 100 na walimu 5 tu. Ni kama haiwezekani kuthibiti na kuendeleza adabu. Utafanyaje kuifanya sehemu hii iwe salama nay a furaha kwa wote, wanafunzi na walimu? Nini mawazo yako? Utachukua hatua gani?

3. Wewe ni mwalimu. Dickson ana umri wa miaka 6. Amekuwa shuleni kwa miezi michache. Mara kwa mara huwa ana pigwa na baba yake mlevi. Mama yake amefariki. Ni mtoto ambaye ana aibu n ani mkimya nah ana ujasiri sana. Asubuhi moja unamuona analia nyuma ya mti. Ana sema ana maumivu. Una ona damu kwenye kaptula yake, na ana majeraha makubwa mwilini mwake. Mkono wake una onekana umevunjika. Ana onekana ana ogopa na hasemi ni nani wala kutoa taarifa zaidi. Je, hili ni tatizo? Kwa nini? Ni nini chanzo cha tatizo hili? Ni nini kitatokea kama haita zuiliwa? Una fikiri Dickson anajisikiaje? Nini kitasaidia hali ibadilike? Kama mkufunzi utafanya nini?

. **Mrejesho**: sikiliza majibu na mawazo ya kila mmoja. Ongezea kama ni lazima.

1. Uko kwenye kikundi cha kwaya cha kanisa na mnafanya mazoezi kila ijumaa. Kuna mwanamke anaitwa Helena ambaye mara kwa mara humleta Felista, binti yake wa kambo mwenye miaka 7. Unagundua kwamba wiki chache kadhaa Felista amekatwa na ana majeraha kwenye macho yake. Nini kinaendelea kwenye mawazo yako/ ungefanya nini? *(labda mama yake wa kambo ana mtesa? Au inaweza ikawa mtu mwingine. Unaweza kuzungumza na Felista kwa upole na kumuuliza. Kama Felista atakwambia nani ana mpiga unaweza kutafuta namna ya kuzungumza na huyo mtu au mtu mwingine kwenye familia).*

2. Kanisa lako linasimamia klabu ya Biblia wakati wa likizo ya pasaka. Kuna watoto 100 na walimu 5 tu. Ni kama haiwezekani kuthibiti na kuendeleza adabu. Utafanyaje kuifanya sehemu hii iwe salama nay a furaha kwa wote, wanafunzi na walimu? Nini mawazo yako? Utachukua hatua gani? *( hakikisha watu wazimazaidi au watoto wakubwa wasaidie; zungumza na Mchungaji; kama huwezi kuibadilisha, hakikisha kwamba walimu wote wanafanya kazi kwa pamoja kutengeneza sheria na kuhakikisha watoto wanakuwa watii; chezeni michezo ambayo inamuhusisha kila mmoja kwenye makundi; imbeni nyimbo ambazo zina vitendo na muwafanye watoto wawe wanajishughulisha na kutumia nguvu zao; usiwa karipie-ongea kwenye sauti ya chini yenye nguvu; tumia filimbi kupata usikivu wao.*

3. Wewe ni mwalimu. Dickson ana umri wa miaka 6. Amekuwa shuleni kwa miezi michache. Mara kwa mara huwa ana pigwa na baba yake mlevi. Mama yake amefariki. Ni mtoto ambaye ana aibu n ani mkimya nah ana ujasiri sana. Asubuhi moja unamuona analia nyuma ya mti. Ana sema ana maumivu. Una ona damu kwenye kaptula yake, na ana majeraha makubwa mwilini mwake. Mkono wake una onekana umevunjika. Ana

onekana ana ogopa na hasemi ni nani wala kutoa taarifa zaidi. Je, hili ni tatizo? Kwa nini? Ni nini chanzo cha tatizo hili? Ni nini kitatokea kama haita zuiliwa? Una fikiri Dickson anajisikiaje? Nini kitasaidia hali ibadilike? Kama mkufunzi utafanya nini? *(hili ni tatizo kubwa; zungumza kwa ustaarabu na kwa upole na Dickson, mkalishe chini na umpatie chai au maziwa; muulize nini kimetokea; mwambie utahitaji kumpeleka hospitali kuungalia mkono wake; utahitaji kuongea na polisi au afisa ustawi wa jamii kwanza; fanya uchunguzi wa familia; shule ina ushawishi gani. Hakikisha una msaidia Dickson kwa upole na huruma)*

**Hitimisho:**

Baadhi ya hali zinaweza kuonekana haziwezekani. Kama kuna kazi nzuri ya ustawi wa jamii au mfumo wa ulinzi wa mtoto basi utatakiwa kufanya kinachohitajika. Ila usiache kujali! Lazima kuna kitu tunaweza kufanya mambo yakawa salama. Tunahitaji kutumia ubunifu wetu na akili zetu kutafuta namna nzuri za kuwaadabisha watoto. Hakikisha unajua ni rasilimali gani zinapatikana kwenye jamii yako.

Kwenye somo linalo fuata tutaangalia juu ya uadabishwaji chanya.

***Maombi ya kufunga**: Bwana asante kwa kuwa una warudi wale uwapendao, lakini pia wewe ni mwema na mpole. Tusaidie tuwasaidie watoto wanaoteseka na ukatili na hofu kwenye Maisha yao. Amina*

## Somo la nane: Uadibisha wenye afya wa watoto

**Lengo**: watoto wana hitaji kuadabishwa! Lakini adhabu kali zina wadhuru watoto. Uadabishaji mzuri unamsaidia mtoto kukuwa n ani kwa faida yao.

**Kivutio**: tafakari kama wewe ni mtunza bustani unaye jaribu kufanya mimea yako istawi. Wakati mwingine ina kubidi uyakate majani na matawi yaliyo kufa ili mmea ustawi na uzae matunda na maua mengi. Je, mtunza bustani ana jaribu kuuharibu mmea? Hapana. Ana ufanya ustawi na uwe una zaa zaidi.

**Ujumbe muhimu**: kama unakipenda kitu una kitunza, una kiadabisha na kukisaidia kukua.

**Mstari wa Biblia**: Waebrania 12:4-10. Mwanangu usiyadharau marudia ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye; maana yeye ambaye Bwana ampenda humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubalie. Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiye rudiwa na babaye? Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali. Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi.

### Funzo kuu

Adabu ni nini. Adabu ni njia mtoto aliyo fundishwa na kuongozwa. Inajumlisha sheria na maonyo. Wazazi wazuri huwaadabisha watoto wao. Mtoto ambaye haadabishi anaweza kujisikia kutokupendwa na kutokujaliwa. Kwa mfano, Yohana akichelewa kurudi nyumbani kutoka shulemi hakuna anyejali wala kuonyesha kuliona hilo. Rafiki yake Briani anatakiwa kuwa nyumbani kabla giza halija ingia na kama akichelewa baba yake humuadhibu kwa kutokumruhusu kutumia sukari kwenye chai yake. Briani haifurahii adhabu lakini anajisikia kupendwa na kujaliwa.

Kisa mafunzo: 

Daudi na Andrea ni mapacha. Wana umri wa miaka 8. Wanaye dada yao. Baba hukasirika sana kwa sababu ana wasiwasi hakuna fedha na mwajiri wake ni mkali sana. Baba akirudi nyumbani jioni ana mgombeza mama yao na wakati mwingine humpiga. Mtoto huwa analia san ana hili humfanya baba akasirike Zaidi. Wiki iliyopita Daudi alidondosha sahani iliyokuwa na chakula na baba alikasirika. Alichukua fimbo na kumpiga Daudi kwa nguvu kichwani. Daudi ana jeraha kubwa na kichwa kina muuma.

- Una fikiri kwa nini baba alimpiga Daudi?
- Je, Daudi alifanya kosa lolote?
- Je unafikiri kwa nini baba ana hasira sana?
- Ni nini hatari ya hasira yake?



**Kikundi kidogo: jadili maswali haya**

Uliadhibiwa vipi na wazazi wako?
Una fikiri adhabu za kimwili ni jambo zuri? Kwa nini ndio au kwa nini hapana?
Biblia inaposema usimnyime mtoto mapigo na kumuharibu ina maana nini?
Biblia inaposema uwapo na hasira usitende dhambi, ina maana gani?
Kuna faida gabi za kumpiga mtoto? Kuna hasara gani za kumpiga mtoto?
Unaijua tofauti kati ya kumpiga mtoto na kumnyanyasa? Tofauti ni ipi?

**Kupiga watoto kunaweza kusababisha madhara kwenye miili yao.**
Kuna maarifa yanayo endelea kwamba kutumia ukatili kumuadhibu mtoto sio kumsaidia na inaweza kuleta hatari hasa mtu mzima anapokuwa na hasira au amelewa. Kupiga watoto usoni au mikononi kunaweza kusababisha madhara ya milele. Inaweza kuwa ni jinai kwenye nchi yako.

**Kuwapiga watoto kunaumiza mioyo yao.**
Kusababisha maumivu huleta hofu. Watoto hawawezi kujifunza wakiwa na hofu.

**Kuwapiga watoto husababisha wawapige watoto wengine**
Watoto hujifunza kutokana na kile wanacho on ana kupitia.

**Kuwapiga watoto kuna maanisha watatii kuepuka maumivu**
Lakini haibadili mioyo yao.



Kwenye hali ya daudi na Andrea- ni nini jibu la hasira ya baba yao?
Tatizo linaweza kutatuliwa vipi?



Mmepata majibu gani? (hakuna majibu marahisi kwenye hili maana kila familia ni tofauti. Labda mtu mwingine – Mcungaji au ndugu- anaweza kuzungumza na baba na kueleza jinsi ilivyo hatari kumpiga mtoto kichwani).

Shule
Shuleni, watoto hupigwa kama adhabu. Kuna njia nyingine za kurekebisha tabia lakini zinahitaji nguvu kubwa kurekebisha tabia!

Wakati wakubili tabia mbaya, mfano rahisi wa tabia, ambao hutumiwa mara nyongi na walimu shuleni, umaweza kufanya kazi kwa ufanisi.

Hii hapa ni mifano rahisiz,

1. maneno ya kimya
2. uchaguzi
3. matokeo

**Maneno ya kimya:**
Kuwa na muda tulivu na mtoto kwa kumuuliza mtoto kwa nini ana tenda katika njia hii na uelezee umuhimu wa kusahihisha.

**Uchaguzi**: kama tabia itaendelea kuwa changamoto mpe mtoto nafasi ya kuchagua. Kwa mfano, sema "unaweza kuchagua. Unaweza kuchagua kubadili tabia yako ama sivyo, kutakuwa na adhabu"

**Matokeo**:kwa pamoja kama walimu mna hitaji kujadili ni adhabu gani mnaweza kutumia ambayo inafuata kanuni za upendo, heshima na ulinzi wa mtoto. Kitu kingine cha kukumbuka kutambua mwanafunzi anapokuwa na tabia njema. Kuwa wazi unapo msifu ili ajue kwa nini wana sifiwa. Kwa mfano, " asante Daudi kwa kukaa kwa kutulia na kusikiliza vizuri. Unafuata sheria za darasa letu vizuri"

Hii hapa ni rasilimali nzuri kwa ajili shule .https://raisingvoices.org/resources/gst-positive-discipline-poster/

## Hitimisho

- Kuadabisha maana yake kufundisha na kuelekeza kwa njia ya sheria na mipaka.
- Adhabu ni kutoa onyo/ fundisho au kupiga faini kwa kosa lililo tendeka (kwa mfano: kuondolewa kwa upendeleo fulani, au matokeo ya kimwili kama kutokupewa chakula, au fimbo)
- Adhabu zote na kuadabishwa kote iwe ni dhumuni la kumfundisha mtoto kuchagua kufanya jambo lililo sahihi. Hofu na maumivu sio vishawishi vizuri kabisa kuleta mabadiliko ya tabia.
- Uadabishwaji chanya na zawadi unahamasisha watoto kutaka kufanya kitu sahihi na kutaka kufanikiwa


***Maombi ya kufunga**: Bwana Mungu, asante kwa kuwa unatuadibisha kwa ajili yetu wenyewe, tafadhali tufunndishe namna nzuri ya kuwarudi watoto bila kuwavunja mioyo na kuwakatisha tamaa. Tupe hekima na ujasiri kusimamia kilicho sawa. Amina*

## Somo la tisa: Unyanyasaji wa kihisia

**Lengo**: kuelewa matokeo ya muda mrefu ya majeraha yasiyo onekana.

**Kivutio**: tafakari juu ya saruji iliyolowa ambayo hutumika wakati wa kujenga msingi wa jengo. Kinatokea nini mtu anapotembea juu ya saruji mbichi? Huacha alama za miguu ambazo ni za milele.

**Mawazo muhimu**: akili za watoto ni laini nab ado zinakuwa. Wanakumbuka kilicho semwa na jinsi walivyo jisikia. Leo tunapo zungumzia kuhusu unyanyasaji wa kihisia, tunazungumzia kuhusu maneno ambayo husemwa kwa mtoto ambayo huweka alama inayobaki kwa miaka mingi sana.

### Fundisho kuu 

**Unyanyasaji wa kihisia na kiakili**

Hii inajumuisha lugha na mashitaka dhidi ya mtoto ambayo yalifanywa na mtu mzima ambayo ni yakuaibisha na husababisha aibu na hofu. Kumfanya mtoto kuwa mbuzi wa kafara ili wajisikie si kitu; kupiga kelele na kuwanyooshea vidole kwa hasira; kumpuuza au kumuepuka mtoto kwa sababu fulani; kuwatishia kuwadhuru au kuwatelekeza; kuwahonga ili watunze siri kuhusu jambo fulani.

Uhalisi: unyanyasaji wa kihisia una madhara makubwa sana kwa watoto na unaweza kumuathiri akili/ uelewa wake, maendeleo ya kielimu na kimwili kwa njia nyingi. Watoto wanapopitia msongo wa mawazo sugu homoni chochezi kama adrenalin na Cortisol huongezeka katika kiwango chao cha damu. Homoni chochezi hizi zina athiri mfumo wa kinga za mwili na kusababisha magonjwa kama vile vidonda vya tumbo, maumivu ya kichwa, shinikizo la juu la damu na maambukizi.

Maandiko yanasemaje?

Mungu huwapokea watoto kama walivyo na kuwatendea kwa upole. Marko 10:13-16

Watu welevu wanaweza kuzuia hisia zao na hawatendi kwa hasira Mith 29:11, Yakobo 1:19

Maneno yanaweza kuumiza na maneno yanaweza kuponya Mithali 1:18

Watu welevu wamejaa huruma na tunda jema Yakobo 3:17

Tunda la Roho kwenye maisha yetu linaonyesha wema, uzuri, uvumilivu, kujizuia Gal 5:23

*Kumbuka watoto wanachohitaji kushamiri. Kutiwa moyo, kuthibitishiwa, ulinzi, mipaka, uthabiti.*

> Unyanyasaji wa kihisia ni pale mtu anaposababisha madhara kwenye nafsi, moyo na fikira za mtoto kwa sababu ya maneno waliyo zungumza na namna walivyo zungumza.

- Hii inaweza kuwa kwa kumdhalilisha mtoto: wewe ni mjinga, huna thamani, hakuna anaye kupenda.
- Kwa kusema maneno ya kikatili, kama vile 'nitakutoa nje ya nyumba'.
- Kwa kuwatishia, nitakupiga, nitakukata mikono yako.
- Kwa kuwatenge na kuwapuuza/ kutowajali.
- Kwa kumfanya mtoto kuwa 'mbuzi wa kafara' wa familia. Mtoto analaumiwa kwa kila kitu.
- Kuwacheka na kuwafanya wajisikia aibu.

Tafakari kuhusu Biblia isemavyo kuhusu ulimi. Yakabo 3:8 inaufafanua kama sumu. Yakobo 3:6. Ni kama moto. Moto ni kitu kizuri au kibaya?

Ni kama kisu kikali. Kisu kikali ni kitu kizuri au kibaya?
Inategemea na jinsi unavyo kitumia.



**Group work: Kazi za kundi**

- Zungumzia kuhusu utoto wako mwenyewe na namna watu wazima walivyo zungumza na wew na kukutendea.
- Toa mifano chanya na hasi ya namna ulivyokuwa ukitendewa.
- Ni yapi matokeo hasi ya ubaguzi?
- Ni yapi matokeo chanya ya kuthibitishwa?

**Hitimisho:** 

Kamwe usidharau nguvu ya maneno. Ftafakari kuhusu watoto ambao ungewatia moyo na kuwathibitisha. Ni jambo gani unaweza kulibadilisha leo kuboresha namna unavyo zungumza na watoto?

**Maombi**: Baba tafadhali nisaidie kutumia maneno yenye kubariki na kuwajenga wengine. Amina.


## Somo la kumi: Utelekezaji

**Lengo:** kutambua aina tofauti za utelekezaji zinavyo onekana na madhara yake kwa watoto.

**Kivutio**: Tafakari kuhusu mtu anayelima nyanya kwenye bustani yake mwenyewe. Ni ulinzi wa namna gani mmea unahitaji? Kivuli kwa ajili ya jua, udongo mzuri, hakuna konokono wala wadudu. Kama ukiuacha tu, utaharibika kutoana na mazingira.

**Mawazo muhimu**: Watoto ni wategemezi kwa watu wazima kwa ajili ya kupata mahitaji yao.

**Mistari ya Biblia**: Mara zote upendo hulinda, huamini, hutumaini na huhifadhi. 1 Kor 13:17

### Fundisho kuu 

Mtoto bado anakuwa na ana hitaji kuhudumiwa kama mmea mdogo. Utelekezaji ni pale mtoto anapoteseka kwa kukosa mahitaji muhimu kwa sababu ya kukosa matunzo. Si sawa na mzazi ambaye ni maskini sana kwamba hawawezi kuwapa mahitaji. Kwa mfano: Mama Josefina anaishi kwenye mazingira magumu sana; ana watoto wane na mume wake alimwacha. Anatumia siku nzima kuuza vitunguu pembeni mwa barabara. Watoto hula chakula mara moja tu kwa siku. Mara zote huwa ana hakikisha watoto wake wamekula kabla yeye hajala. Wakati wowote awapo na fedha kwa ajili ya mayai huwa anawapa watoto wake. Je, huu ni utelekeaji? Hapana!

Kumbuka tulicho zungumzia kabla: watoto wanahitaji nini?

*Kimwili*? Chakula kizuri, protini, maji, kukuwa, ulinzi, afya, chandarua cha mbu, maji safi, usafi wa mazingira (choo), makazi, usafi

*Kihisia*? Kujisikia kuwa sehemu ya, kutiwa moyo, kuthibitishwa, kujisikia salama, kulindwa

Ina maana gani kuwa mbuzi wa kafara?

Kufanywa mbuzi wa kafara: hii ni pale mtoto anapotengwa na kutendewa vibaya na walezi wake. Inaweza kutokea kama mtoto ana ulemavu, au sio mwelevu, au ni mtoto aliyeletwa kutoka nje ya familia ( kwa mfano mtoto wa kambo au ndugu) au

kutoka kwenye ukoo au kabila tofauti. Kufanya mbuzi wa kafara ni ubaguzi wa mtoto.



**kazi ya kundi:**

**Daudi**

Daudi ana umri wa miaka 9; ni moja kati ya wanafunzi wako wazuri. Mama yake amefariki. Ana ishi na baba yake. Baba yake ameoa mwaka uliopita. Mama wa kambo wa Daudi ana watoto wane. Toka baba yake amefunga ndoa, silika ya daudi imebadilika. Nguo zake ni chafu. Daudi amepungua uzito- anaonekana amekonda na hana furaha. Alama zake za shule zimeshuka. Amekuwa akiiba chakula kutoka kwa wanafunzi wenzake. Swali la kujadili: Je, hili ni tatizo? Kwa nini? Ni zipi sababu za tatizo hilo? Ni nini kitatokea kama tatizo halitaisha? Una fikiri Daudi anajisikiaje? Nini kitasaidia hali hii kubadilika? Kama Daudi angelikuwa ni mwanafunzi wa shuleni kwako, ni ishara zipi zingeonyesha kwamba kuna tatizo?

**Hitimisho**: sikiliza Biblia inasema nini kwenye kitabu cha Mhubiri 4:1. 'kisha nikaona udhalimu wote unaofanyika duniani. Watu wanao kandamizwa hulia machozi, lakini hakuna yeyote anaye wafariji'. Utekelezaji wa mtoto ni pale mtu mwenye nguvu hafanyi chochote kumsaidia mtoto. Wapi unaweza kutambua hili na kuzungumza kwa niaba ya mtoto anaye kandamizwa. Unawezaje kuwafariji?


***Maombi ya kufunga**: Baba, fungua macho yetu tuone huzuni na maumivu yanayo tuzunguka. Tusaidie kuwafariji wengine na kutafuta njia za kuzungumza kwa ajili ya walio kandamizwa. Amina.*

## Somo la Kumi na moja: Unyanyasaji wa kingono

**Lengo**: kuelimisha juu ya aina ya unyanyasaji wa kingono na kuwasaidia watoto kupata msaada.


**Kivutio:** takwimu zinatuonyesha kwamba 1 kati ya wasichana 4 na 1 kati ya wavulana 6 wamefanyiwa unyanyasaji wa kingono utotoni mwao. Hii inamaanisha kwamba kati ya wasichana 100, wasichana 25 wamefanyiwa au watafanyiwa unyanyasaji wa kingono. Na wavulana 16 kati ya 100. Hili ni tatizo kubwa na litawa athiri wengi kwenye chumba hiki kutokana na walichopitia wao wenyewe. Tuombe mwanzoni mwa skipindi hiki kwamba mioyo yetu ilindwe tunapo jifunza.

**Mawazo muhimu**: unyanyasaji wa kingono kwa mtoto ni tendo lolote la kingono au aina ya kuguswa ambapo mtoto anatumiwa au kunyonywa na mtu mzima au mtoto mkubwa kwa dhumuni la ngono. Inaweza kuwa mguso, kutokuguswa, kwa kuona au mtandaoni.

**Funzo kuu** 

Kumbuka tulicho kisema kuhusu watoto na walivyo wepesi kukubali na kuamini. Wanahitaji kulindwa.

Unyanyasaji wa kingono: ni pale mtu mmoja anapo mnyonya au kumtumia mtoto. NI UCHAGUZI AMBAO MTU HUFANYA KUMNYANYASA MTOTO. Sio jambo linalo tokea kwa kutofuata kudhamiria. Watu wana maamuzi yakufanya. Hata kama shetani husababisha dhambi, bado ni UAMUZI wa mtu kutenda kwa tamaa zake. mara zote ni mbaya kwa mtoto kunyanyaswa. Mtoto sio wakulaumiwa.



Unyanyasaji wa kingono kwa mtoto ni kumuhusisha mtoto kwenye shughuli za kimapenzi pamoja na mtu mzima au mtoto mwingine ambayo inajumuisha:

- Mguso wa kimwili: kukutana kimwili (au kuingiza uume, vidole au sehemu nyingine ya mwili au kitu) na sehemu za siri za muhanga zilizo funikwa na nguo au bila nguo, matako, kumshika au kumbusu mtoto kwa lengo la kujiridhisha kimapenzi.

- Kwa maneno: semi ambazo zinajumuisha vitisho vya kimapenzi, (iwe ana kwa ana, kwa njia ya mtandao au kwa mitandao ya kijamii), au maelezo yoyote kwa maneno yenye lengo la kuamsha hisia au kuleta msisimko wa kimapenzi.

• Kwa kuona: kujionyesha utupu, kuonyesha mambo ya kingono au kuonyesha sehemu zako nyeti, kumchunguza mtoto kwa lengo la kimapenzi au kumfanya mtoto avue nguo zake ili kuwachukua picha mjongeo (video) au kumchukua picha.

• Madhara ya ngono kwa njia ya mtandao: maduka yanayowezesha upatikanaji wa mtandao, au matumizi ya simu janja kuangalia au kutuma picha au jumbe za ngono. WhatsApp, TikTok, Instagramu, mtandao wa Facebook, Telegramu) yaweza kuwa mazingira ambapo madhara ya kingono hutokea.

- Unyanyasaji wa kingono kwa watoto umesambaa sehemu kubwa na hutokea kwenye kila nchi na kila tamaduni. Suluhisho mara zote huwa si dhahiri na hutofautiana kulingana na hali husika. Kuwa na busara na ujasiri[ii] ina maana kwamba tunahitaji kuchagua kwa umakini nini cha kufanya ili kumsaidia mtoto na sio kufanya hali iwe mbaya/ ngumu kwao[3]

<u>Children who have been sexually abused may</u> ☹
<u>watoto walionyanyaswa kingono wanaweza:</u>

- kujilaumu
- kujikatia tamaa, kuishi na hali ya woga au hofu
- kujisikia hatia na aibu
- Kuchukia miili yao
- kuogopa tendo la ndoa wawapo wakubwa
- kujihusisha na kazi za hatari sana
- kupoteza tumaini
- kujisikia hawapendi au wameachwa na Mungu

Unyanyasaji mara zote unahusu utumiaji mbaya wa madaraka wa mkosaji na kutokuwa na nguvu kwa muhanga. Sio kosa la muhanga! Fikiria kuhusu wakati ulipokuwa mtoto na kujisikia kama huna nguvu.

Sasa tunakwenda kuangalia baadhi ya mifano ya watoto waliokuwa wahanga kwa kukosa nguvu ambapo iliwasababishia kunyanyaswa.



**Kazi za kundi:**

*Kila kundi lipokee kisa mafunzo. Wape dakika 30 za kujadili. Mtu mmoja atawasilisha majibu.*

*"tafadhali kumbuka kwamba kunawezekana kusiwe na jibu moja sahihi! Ufumbuzi wote unategemea na muktadha na kukumbuka kufanya kitu kilicho bora kwa ajili yam toto alliye kwenye mazigira hayo. Hivyo jisikie huru kutoa mawazo yako na jaribu kuona nini ungefanya kama hili lingetokea kijijini kwako, kwenye jamii yako, kanisani au shulei kwako"*

**Magreti**

Magreti anaishi na mama yake. Ana miaka 12. Mjomba wake husaidia kulipa ada yake ya shule. Pale mjomba wake anapokuja mjini huwa anakaa nyumbani kwao na Magreti pamoja na mama yake. Huwa anakunywa sana pombe na anapolewa huwa anakuwa karibu san ana Magreti. Mara ya mwisho alikuja wakati mama yake Magreti hayupo alimuita Magreti na akamwambia amguse sehemu zake za siri. Alimpa shilingi 200. Magreti alikubali kwa sababu hakujua nini chakufanya.

Mjomba atakuja tena wiki ijayo.

- Je, huu ni unyanyasaji, kama ndivyo, ni aina gani ya unyanyasaji?
- Je, Magreti afanye nini?
- Amwambie mtu? Ni nani amwambie?
- Ni zipi faida na hasara za kumwambia mtu?
- Kama ungelikuwa Rafiki wa Magreti, ungemshauri nini?

**Petro**

Petro ana umri wa miaka 10. Ni yatima anaye kaa Burundi. Alikuwa akiishi na bibi yake mpaka mwaka jana alipo fariki. Aliishi mtaani eneo la Bujumbura kwa miezi miwili kisha akaumwa na akalala kwenye blanketi pembeni mwa mtaa na kuanza kuomba. Alionwa na Bi. John, ambaye alikuwa akipita kila siku. Bi. John alikuwa mwanamke mkarimu. Aliona kwamba Petro ni kijana mwelevu. Alimwezesha Petro kupata ufadhili kwenye shule ya bweni ambayo alikuwa akifundisha. Petro alikuwa akiishi kwenye chumba cha mbweni kimoja na wavulana sita. Jana usiku wavulana wawili wakubwa- Eriki na Henry- walimshika Petro kwa nguvu na kumlazimisha alale chini kwa tumbo wakati wakiivuta chini kaptula yake na chupi yake. Kisha walikaa juu yake kama wanaendesha punda. Walimcheka. Wavulana wengine walikuwa wakiangalia. Eriki alimwambia Petro kuwa huwa wanafanya hivi kwa wageni wote. Eriki alimwambia kuwa akimwambia mtu yeyote wataweka sumu kwenye chakula chake. petro anaona aibu na anaogopa. Wakati alipokuwa mtaani baadhi ya wavulana wakubwa walimfanyia vitu vibaya. Hataki kurudi mtaani tena ila sasa anafikiri atakimbia.

**Maswali ya kujadili:**

- Kwa nini Petro alikuwa kwenye hali dhaifu hata kabla ya kujiunga na shule ya bweni?
- Unafikiri ni kwa nini wavulana walichagua kufanya jambo hili kwa Petro?
- Unafikiri ni kwa nini Eriki na Henry wanatenda hivi? Kwa nini wavulana wengine walikuwa wakiangalia tu bila kumwambia mtu yeyote?
- Petro afanye nini?
- Je, amwambie mtu?
- Kwa nini anaweza kuamua kutokumwambia mtu yeyote? Nani anaweza kumwambia?
- Ni watoto gani wengine wanaweza kuwa hatarini? Kama Petro atamwambia Bi. John (mkufunzi) ni kitu gani Bi. John anatakiwa afanye?
- Shule inaweza kufanya nini kupunguza hatari zinazo fanana na hii kwa watoto?

**Gloria**
Gloria ana umri wa miaka 13, anasoma katika shule ya Sunshine. Ni mwanafunzi mzuri. Anaishi na dada yake na mama yake. Wiki iliyopita mwalimu wake Bw. Edwini alimwambia abaki peke yake baada ya vipindi vya darasani. Aliongea vizuri san ana Gloria. Alirudisha kazi zake za nyumbani na alikuwa na alama nzuri sana. Kisha akamwambia 'njoo karibu'. Alimshika nywele zake na uso wake kisha akamsugua mgongo wake. Gloria hakujisikia vizuri. Bw. Edwin akasema 'wanafunzi wazuri wanapata alama nzuri …. Na siunahitaji alama nzuri, sivyo?' Alimwambia kuwa anataka amfundishe masomo binafsi ya ziada. Alimwambia arudi Jumanne ijayo kwa ajili yakumpa zaidi masomo binafsi ya ziada.

<u>Maswali ya kujadili:</u>

- Bw. Edwini amefanya kosa gani?
- Kwa nini Gloria hakumwambia aache?
- Gloria afanye nini sasa?
- Kama akimwambia mama yake, mama yake atafanya nini?
- Kwa nini ni vibaya Bw. Edwi kumfundisha masomo binafsi ya ziada?
- Ni nini kitatokea kama Gloria akienda Jumanne ijayo kama ilivyo pangwa?
- Ni nini shule ya Sunshine inaweza kufanya ili kuwalinda wanafunzi dhidi ya unyonyaji?

**Vincent**

Vincent anakaa na dada zake, kaka zake na wazazi wake.wazazi wake wana biashara mjini, wanauza vifaa vya umeme. Vincent ana miaka 13. Wakati wa Krismas baba yake Vincent anampatia kila mtoto simu janja ili waweze kufanya uchunguzi wa masomo yao na kujifunza vitu. Vincent amegundua mambo mengi mtandaoni. Wakati wa usiku akiwa kitandani hucheza michezo jongeo na anaingia kwenye mitandao ya kijamii. Pia huwa anaangalia picha mjongeo za ngono. Anafahamu kuwa anacho kifanya si sahihii ila hawezi kuacha. Anafahamu kuwa akimwambia baba yake, atanyang'anywa simu janja yake.


- Je, ni tatizo? Kwa nini?
- Vincent afanye nini?
- Anaweza kumwambia nani?
- Kama angelikwambia wewe, ungelimsaidiaje?
- Je, unaona hatari za mitandao?
- Kuna hatari gani nyingine zilizopo za ulinzi wa mtoto?
- Tunaweza kufanya nini ili kuwasaidia watoto na tatizo hili?

**Josephina**

Josephina ana umri wa miaka 7. Anaishi na baba na kaka yake. Mama yake alifariki mwaka uliopita. Wanaishi kwenye nyumba ndogo yenye vyumba viwili. Analala kitanda kimoja na kaka yake Patriki. Ana miaka 15. Mwezi uliopita ikiwa usiku wa manane kaka yake alimbusu Josephina mdomoni na kuweka ulini wake mdomoni mwake. Josephina alimwambia aache. Patriki alisema alikuwa anaota tu. Alimwambia asimwambie mtu yeyote au atasema alikuwa ana danganya. Sasa anamshika kila usiku kwenye sehemu zake za siri. Josephina anajifanya amelala. Haelewi nini chakufanya. Anaona aibu na anaogopa.

<u>Questions to discuss: Maswali ya kujadiliana:</u>

- Je, hili ni tatizo? Kwa nini?
- Ni nini sababu za tatizo hili?
- Ni nini kitatokea kama tatizo halite isha?
- Unafikiri Josephina anajisikiaje?
- Unafikiri kwa nini kaka yake anafanya hivyo?
- Ni nini kinaweza kufanyika ili kubadili hali iliyopo?
- Kama Josephina angelikuwa ni mwanafunzi darasani kwako, ni alama gani zingekuonyesha kuwa ana tatizo?
- Kama Josephina atawaambia walimu, ni nini wanaweza kufanya?

 **Mrejesho**

Tusikilize kutoka kwenye makundi na tuone mmekuja na majibu gani*? Hakikisha anafahamu kwa nini wamefanya maamuzi waliyo fanya.*

**Ujumbe muhimu**:wakati mwingine unaweza kuhisi kama hakuna chochote kinaweza kufanyika. Lakini kumbuka kuna kitu unaweza kufanya. Jambo moja la muhimu ni kumwambia mtoto anaye nyanyaswa, ‘ hili sio kosa lako’.

**Kisa mafunzo kilicho pitiwa tena:**

**Petro.**

Petro aliamua kumwambia Bi. John kuhusu kilichotokea kati yake na wakina Eriki na Henry. Alikuwa akiogopa nini Bi. John anaweza kusema. Lakini Bi. John alisikiliza vizuri. Alimwambia Petro ‘ pole sana kwa hili lililo kutokea’ Tafadhali niachie mimi. Bi. John alikwenda kuzungumza na msimamizi wa bweni. Msimamizi wa bweni aliamua kuwa haitakuwa sawa kuwaadhibu Eriki na Henry kwa sababu itamletea Petro shida zaidi. Alifahamu pia wote Eriki na Henry walinyanyaswa sana walipokuwa Watoto. Aliamua kwamba leo ndio itakuwa siku ya kuyatoa magodoro yote ya Sunshine na kuyasafisha. Kisha akasema kwamba leo ittakuwa ni siku ya kupanga upya mabweni yote ili kwamba wavulana wadogo watenganishwe na wakubwa. Aliwaambia wavulana kuwa hii itahakikisha wavulana wadogo wanapata usingizi wakutosha na wanalala mapema. Msimamizi wa bweni aliamua kwamba atazungumza na wavulana kila mwezi na kuwaeleza umuhimu wa kutendeana kwa ukarimu na kuwa uonevu hauvumiliki. Lakini pia aliweka sanduku la maoni bwenini kwamba yeyote

mwenye maoni anaweza kuweka maoni yake kama ana jambo la kusema bila kufahamika. Petro alilala bweni tofauti usiku huo, ana furaha na yuko tayari kuendelea kukaa shuleni. Msimamizi amemwambia anaweza kumuona muda wowote akiwa na mashaka.

Think about these questions in your small groups:

Tafakari kuhusu maswali haya kwenye vikundi vyenu vidogo:

- Una fikiri nini kuhusu hili?
- Unakubaliana au haukubaliani na kilicho tokea? Kwa nini?
- Ungefanya nini cha tofauti? Kwa nini?
- Ni watu gani wa muhimu waliosaidia kwenye kisa hiki?
- Busara ya msimamizi wa bweni ikoje kwenye namna alivyo simamia hili?

**Mjumuisho**

- Unyanyasaji wa kinono unaweza kutokea kwa njia zote: kuonana, kutokuonana, kufanywa na mtu mzima au mtoto mwingine.
- Watoto ni kama sisi sote- wao sio ‘malaika wadogo’ na wana athiriwa na tabia za dhambi. Tambua njia ambazo Watoto wanaweza kudhuru au kunyanyasa wenzao.
- Mtoto anapo anza kufanya maamuzi mabaya na kujiingiza kwenye uraibu wa ngono, wanahitaji msaada kubadili njia zao kabla haijafika mbali.
- <u>Mtoto anaponyanyaswa, ni kosa mara zote!</u> Sio kosa la muhanga.
- Suluhisho linaweza kuwa gumu, lakini unahitaji kufanya vizuri bila kuifanya hali kuwa mbaya kwa mtoto.
- Jaribu kufanya maamuzi kwenye kundi dogo au watu wenye busara na wakarimu ambao wanaelewe jinsi hili lilivyo la muhimu.
- Hakikisha unajua kile kilicho kwenye jamii yako mwenyewe: muudo wa wenyeviti 10, ustawi wa jamii; mgogoro wa kubakwa; dawati la jinsia la polisi; mtemi; mawakili wa kienyeji.
- Tumia nafasi zote kuzuia unyanyasaji usitokee. Zielimishe jamii. Wawezeshe Watoto kusema Kimbia, piga kelele! Zungumza! Kama wataweza.

**Tafakari binafsi**

Five minutes: what one thing can you begin to do to be part of the solution?

Fikiria kuhusu: usiri, kutengwa na mamlaka - unawezaje kusaidia kupunguza haya?

Dakika tano: ni jambo gani moja unaweza kuanza kulifanya kuwa sehemu ya suluhisho?

***Maombi ya kufunga:***

*Baba, mwanga wako unatuangazia na unashida giza lote. Tafadhali tusaidie kuileta mioyo yetu mbele zako kwa uwazi na unyenyekevu. Tusafishe na uovu wote. Tusaidie kuipenda nuru kuliko giza, na kuutafuta utakatifu kwa ajili yet una Watoto wetu. Walinde wadogo hawa kwa nguvu za Jina lako. Amina*

## Somo la kumi na mbili: Kuwawezesha watoto kujilinda

(vifaa: mawe matano)

***lengo:*** kuwafundisha watoto kuto piga kimya bali kupiga

**kivutio**: fanya mazoezi – kukimbia papo hapo hatuhitaji kukimbia popote sasa lakini niko sawa ili niweze kukimbia nikihitaji bila kuchoka. Mazoezi hutuweka tayari.

**Mawazo makuu**: wafundishe watoto kabla jambo halijatokea. Wasaidie kupata watu salama wanaoweza kuwasaidia

.


**Mafundisho makuu**

Je, unakumbuka hadithi ya Daudi na Goliathi? Goliathi alikuwa jitu. Daudi alikuwa mvulana mdogo. Unakumbuka jinsi Daudi alivyomuua Goliathi kwa kombeo na jiwe?

Unadhani Daudi aliwezaje kumuua Goliathi kirahisi hivyo?

Tunaposoma 1 Sam 17:34-35 tunaona kwamba Daudi amekuwa na mazoezi mengi ya kuua simba na dubu! Alikuwa mzuri sana hivi kwamba alikuwa tayari kwa Goliathi.

Watoto- ingawa Mungu anatupenda, kuna mambo mengi mabaya duniani. Inabidi tufumbue macho kuona hatari zozote. Tunapaswa kuwa tayari kukimbia na kujitetea.


Daudi alikuwa na mawe matano: 

Tukumbuka mambo matano leo!

1. Mtu yeyote akijaribu kukushirikisha mambo mabaya, kataa.
2. Kama mtu yeyote atakuomba umshike sehemu zake za siri, kataa.
3. Sema Sitaki!
4. Kimbia
5. Mwambie mama au mtu unayemwamini



Mama Sara anampenda mtoto wake.  Amemwambia Sara amwambie kitu chochote na asibaki kimya!



Angalia! Sara anajiamini- anasema SITAKI!

**Hapa kuna hadithi kuhusu Joshua**

Joshua ana umri wa miaka 11 na anaishi na familia yake.  Anapenda kucheza mpira wa miguu katika uwanja mkubwa karibu na nyumbani kwao kila Ijumaa.  Wavulana wakubwa huzunguka baada ya kocha kwenda nyumbani na wanatazama video kwenye simu zao.  Wiki iliyopita Yoshua alikaa huko pamoja nao.  Video hizo ni za watu walio uchi wakicheza na kubusu na kufanya mambo ambayo yanamfanya Joshua ajisikie mchafu na aibu. Anajua ni mbaya lakini pia ana hamu ya kujua na anaendelea kufikiria juu ya kile alichokiona.

Swali: Je, ungempa ushauri gani Joshua anapokwenda kwenye mazoezi ya soka Ijumaa hii?

(anaweza kuondoka mapema na asining'inie/ angeweza kufunga macho yake na kugeuka pembeni wakati wakimuonyesha chochote/ angeweza kumwambia mtu kuhusu hilo/ ni nini kingine anachoweza kufanya?)

Biblia inatuambia kwamba Mungu yuko pamoja nasi sikuzote, akituongoza na kutusaidia.

Zab 32:8 Nitakufundisha njia ikupasayo kuiendea. nitakushauri na kukuangalia.

**KUMBUKA!**

• Mtoto anaponyanyaswa, huwa ni makosa! Sio kosa la mwathirika kamwe.

• Suluhu zinaweza kuwa ngumu, lakini unahitaji kufanya bora uwezavyo bila kuifanya iwe mbaya zaidi kwa mtoto.

• Jaribu kufanya maamuzi katika kikundi kidogo cha watu wenye hekima na wema ambao wanaelewa jinsi jambo hili lilivyo zito.

• Hakikisha unajua kinachopatikana katika jumuiya yako mwenyewe: 10 mwenyekiti wa seli; ustawi wa jamii; mgogoro wa ubakaji; dawati la jinsia la polisi; mkuu; mawakili wa ndani.

• Tumia kila fursa ili kuzuia unyanyasaji kutokea. Fahamu jamii. Wawezeshe watoto kusema SITAKI! Kimbia! Kusema!

*Tafakari ya kibinafsi: Dakika tano:*

*Fikiria kuhusu: usiri, kutengwa na mamlaka - unawezaje kusaidia kupunguza haya?*

*Ni jambo gani moja unaweza kuanza kufanya ili kuwa sehemu ya suluhisho?*

***Maombi ya kufunga:***

*Baba, nuru yako inatuangazia na kulishinda giza lote. Tafadhali tusaidie kuleta mioyo yetu mbele yako kwa uaminifu na unyenyekevu. Utusafishe na kila dhambi. Utusaidie kupenda giza kuliko nuru, na kutafuta utakatifu kwa ajili yetu na watoto wetu. Walinde wadogo zako kwa uwezo wa Jina lako. Amina*

**<u>Somo la kumi na tatu: Ufunuzi</u>**:

***Lengo***: kujua jinsi ya kusikiliza vizuri ikiwa mtoto anafichua unyanyasaji

***Mawazo muhimu***: mkao wazi, sio kukatiza, lugha ya mwili, huruma

***Kivutio:*** kuna mtu yeyote anajua mfano wa ujuzi mzuri wa kusikiliza ni nini?

 <u>Mafundisho makuu</u>

**<u>Ufunuzi</u>**

Hii ni pale mtoto anapo mweleza mtu kuhusu unyanyasaji au kitu kinachoendelea. Unafikiri ni kwa nini inaweza kuwa ngumu kwa mtoto kumwambia mtu kinacho tokea?

*(shame, for example, Vincent; fear, don't know the words, afraid of consequences, don't really understand it is abuse or that it is wrong, fear they won't be believed- give examples from Gloria, Peter, Josephine)*

*(aibu, kwa mfano, Vincent; hofu, hajui manemo, anaogopa matok kujua jinsi ya kusikiliza vizuri ikiwa mtoto anafichua unyanyasaji, hafahamu kuwa ni unyanyasaji au kuwa ni vibaya, wanaogopa wanaweza wasiaminiwe- toa mifano kutoka kwa Gloria, Yakobo, Josephina)*

**Pale mtoto anapo jaribu kukwambia jambo, ni vizuri kulipokea vizuri! Ukijibu kwa hasira au kutokuamini mtoto hatoongea na wewe tena kuhusu jambo au hilo na kazi au unyanyasaji utaendelea.**

<u>Sikiliza ufunuzi:</u>

- angalia alama ambazo mtotot anataka kuzungumza. (kwa mfano, anakuwa anazunguka-zunguka hapo, anatenda isiyo kawaida …..)
- Wakati wanapoanza kukweleza wataeleza kwa vipande taratibu ….. usiwaharakishe kwa kuwaambia, 'ni nini??, si uzungumze! Fanya haraka! Nimechelewa!
- Kuwa mtulivu, sikiliza, na onyesha ushirikiano.
- Usionyeshe hisia
- Kuwa mkarimu, mtie moyo.
- Sema 'asante kwa kuniambia' ninataka kukusaidia.
- Muhakikishie kwamba anaweza kuzungumza na wewe mara zote.

Utatakiwa kushirikishana na mtu mwingine lakini utatakiwa kuwa na busara na mwenye usiri.

<u>Ni nini chakufanya kinachofuata?</u>

- Tafakari kuhusu mtoto alicho sema.
- Hatari ni ipi na iko wapi?
- Ni nini kinawza kufanyika kuzuia isiendelee
- Mtoto anataka nini kitokee baada ya kukweleza? Zingatia hili.
- Kama ukiingilia sasa, itakuwa sawa kwa mtoto au itamuharibia?
- Nani mwingine uaweza kuzungumza naye?
- Je, hili linahitaji kushitakiwa polisi au kwa ustawi wa jamii?
- Ni ipi hatari kwa mtoto kama ukishitaki?
- Je, wazazi wahusishwe haraka, kwa nini ndiyo au kwa nini hapana?
- Kuwa na kikao na mtu mwingine mwenye busara au watu wengine wawili wenye busara ambao wanaweza kusaidia kufanya maamuzi sahihi.

**Kumbuka kwamba unaweza kuwa mtu salama wa mtoto kumwambia siri. kuwa inapatikana kutoka kwao adn kutoa msaada wako na msaada**

***Maombi ya kufunga**: Bwana Mpendwa, asante kwamba utanisaidia daima kufanya jambo lililo sawa. Tafadhali nisaidie kuwa jasiri na kusema ili kujilinda mwenyewe na wengine. Amina*

## SEHEMU YA PILI

**Kutumia sauti yako kuwalinda watoto**

MAKANISA, WANA HISANI & MASHIRIKA YASIYO YAKISERIKALI (NGO’s**)**

Sehemu hii ni kwa mtu yeyote anaye fanya kazi kanisani au kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile nyumba za kutunzia Watoto, miradi ya vijana au hisani za Watoto.

**Unaweza kuitumia kujielimisha au kufundisha viongozi wengine na watendakazi wa watoto.**

Mara nyingi Watoto unao watunza, kuwaongoza au kufanya nao kazi wanatoka kwenye hali duni. Hii inamaanisha wako kwenye uhitaji zaidi wa msaada na ulinzi.

**Ufahamu**

Kama unaendesha huduma au mradi ambao Watoto wanakuja, basi una wajibu wa kuhakikisha kwamba Watoto hawako kwenye hatari ya madhara au unyanyasaji unao zuilika .

*Kwa mfano: unaendesha kila wiki klabu ya baada ya shule kuanzia saa 9-12 jioni kwenye eneo la kanisa. Wakati mwingine kuna Watoto 20 na wakati mwingine wako 50. Mara kadhaa wavulana wakubwa wanakuja na wanakaa kwenye mabanda ya kuku. Unahisi watakuwa wakionyesha Watoto wadogo picha mjongea zisizo nzuri na zisizo na maadili kwenye simu zao. Huwezi kuthibiti kinacho endelea nje ya muda wa klabu lakini uaweza kuweka ubora na sharia ndani ya klabu.*

Ni mambo gani unaweza kufanya kukabiliana na hali?

1. **Kwa nini Wakristo wanatakiwa kujali kuhusu ulinzi wa Watoto?**

Kama wewe ni taasisi ya Kikristo basi utakuwa au utatakiwa kuwa na <u>mtazamo wa kiinjili.</u>

Injili ni **habari njema**. Kulinda Watoto sio wazo la kimagharibi. Neno la Mungu ni la kiulimwengu kwa karne, tamaduni na lugha zote. Licha ya cahngamoto zote zinazo tuzunguka, kama Wakristo tumeitwa kuzitii kanuni za maandiko.

<u>Maandiko yanasemaje kuhusu Watoto na unyanyasaji?</u>

- Watoto ni binadamu kamili na wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Mwnz 1:28
- Watoto ni zawadi ya Mungu kwetu sisi sote. Zab 127: 3

- Watoto ni ishara ya ufalme. Math 18:2-3
- Miundo ya dunia imevunjika Rum 8:22 na hivyo dhambi iko kila mahali.
- Wote wametenda dhambi (rum 3:23) n ahata Wakristo wanaweza kutenda dhambi dhidi ya watoto
- Shetani anakuja kama mwivi kuharibu Yoh 10:10
- Shetani ni kama mbwa mwitu alijivaisha Ngozi ya kondoo ili kulidanganya kanisa. Math 7:15
- Watoto wanahitaji matunzo maalum na ulinzi Mith 31:8
- Yeyote atakaye msababishia mtoto kujikwaa atajisababishia hukumu kali Math 18:5-6
- Mhub 4:1 wanao onewa hawana mfariji kwa sababu muonevu ana mamlaka yote.
- Mungu hutenda saw ana kwa haki wa walio onewa wote Zab 103:6
- Sisi ni watii wa mamlaka na sheria za serikali zetu. Rum 13:1

Hatuhitaji kutafuta mistari ya Biblia ambayo inazungumza kuhusu Watoto. Tunapo yasoma maandiko, tunatakiwa kukumbuka kuwa **watoto ni watu pia**. Hii inamaanisha kila kitu biblia inacho tuambia kuhusu kutendeana sisis kwa sisi inahusu Watoto. Kwa mfano, kuwa wapole, wenye ukarimu, wawazi, wanyenyekevu na wavumilivu (Kol 3:12).

Tunapo kumbuka kuwa Mungu alituita kutenda kwa haki na kupenda huruma, hii inamaanisha kwamba kuwa na wajibu, maadili na sheria kibiblia ya kuzungumza, kufanya tuwezavyo kuzuia madhaa na kulinda Watoto.

**Unafiki**

Kuwa mnafiki ni pale tunaposema jambo hili na tunafanya lingine. Tuna wawekea wengine viwango vya juu lakini sisi wenyewe hatuvifuati. Kwa mfano tuna waambia watu wengine wafunge na kuomba lakini sisi hatufanyi. Au tuna waadhibu wengine kwa kuiba lakini sisi tunaiba.

Unafiki ni jambo lililo mfanya Yesu akasirike sana na lilimuumiza. Mara kwa mara aliwaangalia viongozi wa dini na alihuzunishwa na mioyo yao migumu. Unaweza kusoma Marko 11 & 12 kuona jinsi Yesu anapinga unafiki. Soma Marko 12:38-40.

Tunapo tafakari kuhusu kulinda Watoto, wapi tunaona unafiki?

Hii hapa baadhi ya mifano:

**Helena** anaimba kila wiki kwenye kwaya ya kanisa na mara kwa mara huenda kwenye ziara kuzunguka nchi. Watoto wake hukaa kanisani na kumwangalia akiimba. “Yesu anapenda Watoto!” lakini nje ya kanisa wakiwa nyumbani,

> Helena ni mwanamke mwenye hasira na husema maneno ya kikatili kwa Watoto wake, kwa vitisho kwamba atawatupa nje ya nyumba.

*Kwa nini Helena anafanya hivi? Kwa nini unafikiri Helena ni mtu tofauti kanisani na nyumbani? Una fikiri Watoto wake wanajisikiaje?*

> **Mchungaji Wiliam** ni muhubiri mwenye nguvu na inaifahamu Biblia yake vizuri. Kila mtu anapenda kumsikiliza na wakati mwingine hufanya uhamasishaji wa kitume mjini. Lakini nyumbani, anapiga mke na Watoto wake. Mke wake Esta anasikia aibu san ana hawezi kumwambia mtu yeyote.

*Unafikiri nini kuhusu hali hii? Umesha wahi kuona aina hii ya unafiki kanisani au kwenye jamii yako/? Una fikiri kwa nini Esta anaona aibu? Utampa ushauri gani Mchungaji Wiliam? Utampa ushauri gani Esther?*

> **Dickson** ni kiongozi wa vijana kanisani na pia ni mratibu wa huduma ya kitaifa ya vijana ya INUKA. Anafundisha na kuandika vitabu vya usafi wa ngono na mabadiliko binafsi. Ana kundi la vijana watogo ambao anawaongoza. Kundi hutembelea makanisa mengine na hualiwa kwenye matukio. Dickson huwaalika wasichana wadogo kwenye chumba chake cha nyumba ya kulala wageni, anawapa pombe za kienyezi na kulala nao.

**Injili inatubadilisha**

Kumbuka, sote tunajifunza, tunakuwa, tunabadilika na kwa neema ya Mungu tunasamehewa. LAKINI Mungu amesema kwamba kama tukiithamini dhambi mioyoni mwetu hatatusikiliza. Kila moja ya mifano ile ni mtu anaye rudia dhambi ile ile ya unafiki bila kupingwa. Wanatumia jina la Mung una kazi ya Mungu kama kisigizio chakusifiwa na wengine. Lakini ndani kuna giza na dhambi. Wakati huo huo, Watoto wanaumizwa na kunyanyaswa. Soma tena Marko 12: 38-40. Hatuwezi kuendelea hivi bila kuadhibiwa.

## Kuzuia unyanyasaji wa kingono kwa watoto kanisani na kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO’s)


**Unyanyasaji ni halisi kwenye makanisa yet una kwenye jamii za Kikristo. Kama tutakataa hili basi hatutaweza kusaidia kuwalinda watoto.**

*Miriam husafisha kanisa baada ya maombi ya asubuhi. Mmoja wa viongozi alimwita ofisini kwake na kumuomba amleee chai. Aliufunga mlango. Na akaonyesha sehemu zake za siri kwa Miriam na kumfanya amshike. Miriam alijisikia aibu na hatia. Alijaribu kukataa lakini alimwambia atapoteza kazi yake. Alimwambia kama akimwambia mtu hakuna atakaye mwamini.*

**Fikiri kuhusu hali hii.**

Kwa nini inatokea? Kwa nini Miriam asimwambie mtu yeyote? Ni upi ushauri wako kwa Miriam? Je, una mifano mingine ya wapi haya yanatokea?

**Unyanyasaji wa kingono unatokeaje? Vitu vitatu vinatakiwa kuwa pamoja: (andika kwenye kila mduara)**



- Mnyanyasaji: mtu Fulani aliye amua au anaye shawishika kumnyanyasa mtoto
- Mhanga: mtoto ambaye hawezi kukataa wala kukimbia
- Fursa: muda na eneo unapoweza kutokea

Panapokuwa na mtu anayetaka kumlenga mtoto +kunapokuwa na mtoto+ kunapokuwa na fursa= hatari kwamba unyayasaji unaweza kutokea.

**Tuangalie kila duara:**

**Mnyanyasaji**: ni aina gani ya mtu anaye mnyayasa mtoto? Anaweza kuwa mtu anaye onekana kawaida kabisa na wa kawaida. Usiwaamini kwa kuwa ni watu wa dini.

**Mhanga**: mtoto asiyejua jinsi ya kukataa au kukimbia. Mtoto mwenye uhitaji wa zawadi kama pesa au chakula.

**Fursa:** namna ya kumopata mtoto akiwa peke yake: kwa siri ambapo hawawezi kuonekana.

Ili kupunguza hatari ni lazima uangalie kila duara moja ya haya! Njia rahisi ya kupunguza hatari ni kuzuia fursa. Hii ina maanisha kuangalia jografia ya mahali husika ya hudum au kazi yako. Biblia inatwambia matendo ya dhambi hufanywa gizani ambapo hakuna mtu anaye weza kuona. Efe 5:11-12

**Sasa fikiri kuhusu kanisa lako mwenyewe au shirika lako.**

- Ni shughuli gani zinaendelea pale? Ziorodheshe.
- Vipi kuhusu shughuli za watoto au wakati watoto wakiwepo
- Ni rahisi kwa mtu mzima kuwa peke yake na mtoto bila kuonekana?
- Kuna sehemu za giza, za siri? Ndani, nje?
- Chumba cha ofisi kina madirisha au milango ambapo unaweza kuona ndani?
- Watoto wanaweza wakalengwa wapi kirahisi? Kwa mfano, vyooni.
- Kuna shughuli zozote ambapo mtoto anakuwa peke yake na mtu mzima ambapo hakuna mtu anaweza kuwaona? Kwa mfano, kuwaendesha kwenda nyumbani au kazi za usiku?

Biblia inatuambia kutembea nuruni. Kwa hiyo hakikisha unapo tembea na watoto hakuna kitu kinacho fanywa sirini. Jiulize mwenyewe, “ inawezekana wengine kuniona?”

Kumbuka kwamba usiri, kujitenga, na giza ni hatari kubwa na lazima uangalie njia zakuepuka na utengeneze uwazi, mwonekano na uwajibikaji.

Hizi hapa ni mbinu zinazo weza kusaidia kuongeza uwazi uwapo na watoto ( haya ni mawazo tu yanayo weza kusaidia, ila unaweza kufikiri zaidi:)

- Yeyote anayetaka kuwa peke yake na mtoto ( kwa mfano huduma ya kwanza) lazima amwambie mtu mzima mwingine wako wapi na kwa muda gani.
- Epuka kuwa na mtoto peke yako kwenye chumba ambacho hakina madirisha.
- Acha milango wazi
- Acha mapazia wazi
- Lenga kufanya shughuli za watoto mchana
- Kutana nao kwenye maeneo ya wazi kwa ajili ya ushauri, kwa mfano kwenye banda ambalo watu wanaweza kuona ila wasisikie
- Kuwa na kazi zenye mtoto zaidi ya mmoja – kwa mfano, masomo ya ziada
- Kama hii ni jambo la ndani au matibabu hakikisha mzazi au mlezi wa mtoto yupo.
- Mwache mtoto akae karibu na mlango, ili wasijisikia zidiwa au kunaswa.
- Usiende chooni peke yako na mtoto ( labda kama ni ndugu)

- Epuka kufanya jambo ambalo unawza kushtakiwa au kukosea.

Hivi hapa ni baadhi ya visa mafunzo:

**Raheli** ni mshauri mpya kwenye kanisa la Victory na mara kwa mara anafanya kazi na wakimbiszi wadogo. Amepewa chumba kwenye ghorofa ya juu ya jengo la kanisa na ameambiwa anaweza kuitumia kati ya saa 11 jioni na saa 2 usiku.

*Kuna matatizo gani ya mpangilio huu? Una fikiri Raheli atoe maoni gani kufanya mpangilio huu uwe salama?*

**Robati** ni mmoja wa afisa ustawi wa jamii kwenye mradi wa watoto wa mitaani wa REUNITE. Mradi huu unafanya kazi kuwaunganisha watoto walio kimbia na watoto wadogo na faminlia zao. Anawapeleke watoto kwenye masafa marefu kurudi kijijini kwao. Mara kwa mara huwa wanalazimika kukaa kwenye nyumba ya wageni kwa usiku na ili pia wahifadhi pesa, Robati anashirikiana chumba na mtoto.

*Kuna matatizo gani yanayo weza kutokea? Unafikiri nini kinaweza kikafanyika kuzuia tatizo lolote?*

**Yosefu** ni Daktari wa viungo na anafanya kazi na kituo cha watoto wenye ugonjwa wa kupooza ubongo na magonjwa mengine kiitwacho HOPE. Familia zinawaleta watoto wao kwenye kituo kwa ajili ya mazoezi na kuwakanda-kanda. Watendakazi jamii wawili pia huwa wanasaidia. Kuna chumba kimoja kikubwa kwa ajili ya watoto kucheza na kuna chumba kidogo ambako Yosefu hufanya kazi zake.


*Unafikiri kwa nini watoto hawa wako duni zaidi ya watoto wengine ambao si walemavu? Yosefu afanye nini ili kuhakikisha kila kitu kiko sawa? Aepuke nini?*

## Kuwashawishi viongozi na makanisa

Unafanya kazi na watoto kanisani, kwenye shule ya Jumapili au kwenye sehemu ya hisani ndogo ambapo unaona kuna tatizo. Lakini unaona kama hakuna anaye jali, utafanya nini? Unawezaje kuwasiliana na viongozi wako ili kuweza kusaidia kutengeneza sehemu salama na bora kwa watoto kukua? Kama we ni kiongozi au uko kwenye nafasi ya ushawishi, unaweza kuwasilisha vipi kwa watu ambao hawana nia?

**Kazi:**

Chora muundo wa Shirika lako



- Ni wakina nani wote wanao juhusishwa?
- Ni wakina nani ni viongozi?
- Kwa mfano, Mratibu, Mkurugenzi mtendaji, Askofu, Wazee, Mchungaji, Kamati, Mratibu wa Mradi, Mwalimu mkuu
- Wanufaika (watu unao wasaidia)
- Wanao fanya maamuzi
- Wafanya usafi, wabeba mizigo, waandaa chai
- Watoto

**Unatosha wapi? Ni ipi nafasi yako?**

- Sio tu mamlaka ya nafasi ndio yanayo husika. Wakati mwingine watu wana mamlaka na ushawishi bila kuwa na nafasi.
- Ni aina gani za mamlaka unazo ziona?
- Hadhi, pesa, taaluma, hulka/haiba, watu unao fahamiana nao ………..
- Ushawishi ni nini? Ushawishi ni uwezo wakuwafanya watu wengine wakubaliane na wewe
- Wakina nani ni washawishi wa kanisa lako au huduma?
- Wanawake? Wazee? Mke wa Mchungaji?

Kwa mfano:

*Bw. Edward ni moja kati ya watu wanao heshimiwa sana kanisani. Bw. Edward ni mwalimu mkuu mstaafu. Anakaribia umri wa miaka 80. Alikuwa ni mzee wa kanisa*

*ila kwa sasa han uongozi kanisani. Lakini Bw. Edward akizungumza kila mtu anamsikiliza.*

**Na wewe je? Una ushawishi gani?**

Ni watu gani wanao weza kukusaidia kupaza sauti yako?

> Swali: ina jalisha nini kwamba viongozi wako wako kwenye makubaliano kwenye umuhimu wa ulinzi wa Watoto?
>
> > Kwa sababu ni wao ndio mamlaka yao ina nguvu
> > Watu wanawajibika kwenye uongozi
> > Wanahitaji kukubaliana na sera na kanuni na kuzitekeleza.
> > Wanaongoza kwa mfano.

Kama uko kanisani au kwenye shirika lisilo la kiserikali (NGO) basi inakubidi ufikiri kuwa na sera na kanuni za maadili.

## UANDISHI WA SERA

**Sera ni nini?**

Sera ni kanuni zinazo ongelewa au kutokuongelewa za knaisa lako au shirika lako (NGO). Hizi zipo hata kama hamziiti sera! Kwa mfano, ‘kanuni za uvaaji’. Kila mtukanisani anafahamu aina gani za mavazi zinakubalika na zipi hazikubaliki kanisani. Kila mtu anafahamu ni aina gani ya mavazi atavaa msibani au kwenye sherehe. Baadhi ya makanisa yana sera za fedha, kwa mfano kwamba pes azote za sadaka ni lazima zihesabiwe na watu wawili. Sera inaweza ikawa haijaandikwa kwenye karatasi lakini kila mmoja anfahamu nini kinatarajiwa.



Una fikiri sera ziandikwe?

- Ni ipi faida ya sera za maneno/ za mdomo ( kwa watu ambaohawawezi kusoma vizuri, zitawasilishwa kwa urahisi)

- Ni ipi faida ya kuziandika chini? (kama huwa unapokea watu wapya mara nyingi ambao huja na kuondoka, inasaidia kuwa na uthabiti; kama unategemea pesa za ufadhili hii mar azote huwa inahitajika.

Sera za ulinzi wa mtoto inaonyesha kujitoa kwako ili kuwatunza watoto salama. Inajumuisha na viwango vyako juu ya nani utampokea kwa ajili ya huduma ya watoto- kwa mfano tabia zao na sifa zao. Inaelezea jinsi gani mtu yeyote mwenye tatizo au wasiwasi kuhusu unyanyasaji anaweza kupata msaada bila kufukuzwa. Mara kwa mara hutoa jina la mtu ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa ulinzi wa mtoto

Sera zinatakiwa kuwa zina huishwa! Sera ambayo imeandikwa na hakuna anaye isoma, kwenye lugha ambayo inaeleweka haina maana! Ni bora kutokuwaa na sera kuliko kuwa nayo ambayo haina maana.

Kama uko kwenye shirika dogo na unafikiri kwamba kanuni zimewasilishwa vizuri tayari basi mnaweza kusubiri kwanza kabla hamjaandika sera. LAKINI kila mmoja lazima awe na kanuni za maadili.



Fikiria kuhusu amri kumi kwenye Kutoka 21. Mungu aliwapa waosraeli kanuni 10 zakufyata. Musa aliziandika chini. Katika njia hiyo hiyo, kanuni za maadili inampatia kila mmoja maelekezo yaliyo wazi ya nini wanatakiwa kufanya na nini wasifanye.

**Ni zipi kanuni za maadili za ulinzi wa mtoto?**

Ni hati iliyo andikwa.

Iko wazi kuhusu kanuni na yatarajiwayo.

Ina maanisha kila mmoja anafahamu nini anatakiwa kufanya kuwalinda watoto.

Ni fupi na rahisi kueleweka.

Kila mmoja anaweza kuiona.

**<u>Kanuni za maadili ya kanisa la Hosanna</u>**

Kanisa ka Hosanna ni sehemu nzuri na bora kwa ajili ya watoto kukua na kujifunza kuhusu Yesu. Ili kuwaweka salama. Hizi ni sheria zetu:

- Watu wazima ni kifano kwa watoto na wanatakiwa wame maumbo bora kwao
- Aina zote za unyanyasaji zinalaaniwa na kanisa hili.
- Ni marufuku kwa mtu mzima kuwa na mtoto peke yako kwenye chumba kilicho fungwa. Acha milango wazi.
- Hairuhusiwi mwanaume kumshauri binti bila uwepo wa mwanamke.
- Kwenye ziara za vijana lazima wawepo watu wazima wa kutosha.
- Hairuhusiwi kwa kiongozi wa vijana kulala kitanda kimoja na vijana.
- Hakuna lugha za mapenzi, au vitendo au maongezi yanyo ruhusiwa.
- Miguso yote ya karibu kati ya mtu mzima na mtoto hairuhusiwi, kwa mfano kugusa sehemu za siri, kupiga, kubusu
- Hairuhusiwi kwa mwalimu yeyote wa shule ya Jumapili kupig]a mtoto. Mahitaji yoyote ya kuadibisha yapelekwe kwa mzazi.
- Hairuhusiwi kwa mwalimu yeyote wa shule ya Jumapili au mzee kumkaripia mtoto au kumuaibisha. Waelekeze watoto kwa uimara ila kwa upole ili wasiogope kujifunza.

Kama ukiona lolote kati ya yaliyo hapo juu tafadhali toa taarifa kwa Bi. Gloria Mugo ambaye anahusika na ulinzi wa mtoto kwenye kanisa hili na anapatikana kwenye namba hii: 0121 12345.

Unafikiri nini kuhusu hizi kanuni za maadili? Umependa nini kuhusu hizi kanuni za maadili? Utaziboreshaje?

**Kuwa wakili wa watoto:**

Mithali 31:8 sema kwa ajili ya wasioweza kujisemea wenyewe.

Ni nini tunaweza kufanya ili tuzuie unyanyasaji kwa watoto?

Tunahitaji kuwa na ujasiri ili tuzungumze pale tunapo ona kitu.

Tunahitaji kuwatia watoto moyo ili washirikishe hofu zao na tuwasikilize.

Biblia inaposema kuhusu jinsi ya kutendeana sisi kwa sisi, kumbuka kwamba vile tunavyo watendea watoto ina maana kwa Mungu!

Tuzungumze kuhusu matumizi mazuri ya madaraka (hasa kwa viongozi) na matumizi mabaya ya madaraka yanaonekanaje.

Kuwa kama Kristo. Ongoza kwa mfano kwa kuwajali watoto. Sote tuna ushawishi mahali fulani. Wewe ni mhubiri- basi hubiri kuhusu hili. Wewe ni jirani, basi fungua macho yako kuona kinacho endelea mahali panapo kuzunguka. Wewe ni mzazi, basi fundisha watoto wako.
Viashiria vya mtoto ambaye ana nyanyaswa au kudhurika:

- alama za mwilini kama michubuko, kuungua, mikwaruzo
- alama za kukatwa na alama za fimbo
- Mtoto anaye ‘shtuka’ pale mtu mzima anapo mkaribia ghafla.
- Alama za kihisia: kurudia tabia za kitoto, kunyonya vidole, kulia, mabadiliko ya ghafla ya hulka.
- kingono: maambukizi, tabia za kingono, kuvua nguo, mimba

**Hatari: hatari kwa watoto kwenye mazingira tofauti-**

- fikiri kuhusu jamii yako
- Hatari ziko wapi?
- shule za bweni
- Kutembea kwenda na kutoka shule
- Watoto wasio na usimamizi
- Ngono
- maduka yanayo wezesha mitandao
- Biashara za watoto
- unyanyasaji wa wasichana wa kazi za nyumbani
- Kwenye vituo vya kulelea yatima
- Kwenye huduma au kanisani
-

**Kufundisha Watoto**

**Wafundishe!**

Sio sawa kwa mtu yeyote kuwagusa tupu zao
Sio sawa mtu yeyote kuwafanya waangalie sehemu za siri au ngono

- <u>Sema hapana</u>
- Kimbia
- Mwambie mtu salama.

**Mtu salama ( mtu anaye aminika)**

Kumbuka kwamba kuishi kwa ukimya na hofu sio vizuri kwa watoto. Mtoto anahitaji awe na mahali pakwenda ili aweze kupata msaada na faraja. Mara zote tambua kuwa mtoto anaweza kuwa anajaribu kukwambia kitu. Usiwe mkali, usiwasukume mbali. Kuwa wakuaminika na mkarimu. Tia moyo na uwe na huruma wakati unapotafuta kupata suluhisho sahihi.

Unaweza kuwa jirani, rafiki, mwalimu au mchungaji. Tunaweza sote kufanya jambo! Kama unajali vya kutosha utazungumza na kuleta mabadiliko. Tuangalie kisa cha Esta na Gloria.

**Mazingira: Kanisani kwa Gloria**

**Hatua ya kwanza**

Esta anafundisha shule ya Jumapili kanisani kwa kina Gloria. Kila wiki kuna kama watoto 50 ukijumuisha watoto na vijana wa miaka kumi na kuendelea. Huwa kuna walimu wawili wa shule ya jumapili ila wakati mwingine dharula hutokea na mmoja haji. Watoto wadogo wanakuwa wakishangaa ndani na nje ya darasa. Wazazi wao wako kwenye misa ya kanisani. Lakini baadhi ya Watoto wanakuja kutoka jirani.

Mwezi uliopita wakati wa msimu wa mvua mtoto wa miezi 18 alikutwa amedondokea kwa uso kwenye shimo nje ya darasa, alikaribia kuzama ila alivutwa na mmoja kati ya watoto wakubwa na baadaye alikuwa salama. Hakuna aliye onekana kujali sana na wakasema tu Bwana asifiwe, Mungu anatulinda.

Tafakari: ni hatari zipi tofauti kwa watoto walio kwenye hii hali?
- What are the obstacles to change?
  Ni vipi vizuizi vya mabadiliko?
  Ni zipi changamoto binafsi za Esta?
  Anaweza kufanya nini?

**Hatua ya Pili:**

Esta alizungumza na baadhi ya walimu wa shule ya jumapili na wakaomba kuzungumza na mmoja wa wazee, Eriki ambaye pia ni mzazi wa Watoto sita kwenye shule ya Jumapili. Kwa pamoja walikuwa na kikao na wakazungumza na Mchungaji kuhusu mashaka yao. Mchungaji alisema kwamba changamoto ni kwamba watoto wengi kutoka nje ya kanisa wanakuja kwenye shule ya jumapili lakini pia hii ni

baraka na nafasi ya kuwa mashuhuda kwao. Alisema itakuwa vizuri kuwa na walimu zaidi. Atalitangaza kanisani, na alifanya lakini haraka sana katikati ya matangazo mengine.

Mwezi mmoja baadae hakuna kilicho badilika. Hakuna aliye jitolea kutoa msaada kwa shule ya jumapili. Esta amechanganyikiwa. Wiki iliyopita, mwalimu mwenzake alikuwa anaumwa hivyo Esta alikuwa peke yake na watoto 70 walikuja kwenye shule ya Jumapili. Ilimbidi atumie fimbo kuwathibiti baadhi ya Watoto ambao walikuwa wasumbufu. Anafahamu kuwa hii sio nzuri lakini haoni njia nyingine. Anajisikia kama anakata tamaa.

> Unafikiri ni nini kitatokea kama hakuna kitakacho badilika?
> Esther afanye nini sasa?

**Hatua ya 3.**

Esta alimuomba Mungu ampe msaada na hekima. Kisha alimkumbuka mwanamke mwingine, Maria ambaye anauza maua kwenye kona. Maria anasali kanisa tofauti hivyo wakati mwingine Esta alipopita pale alisimama na kumuuliza kuhusu shule ya Jumapili ya kanisani kwao. Maria akamwambia ndani ya wiki tatu walikuwa na siku ya semina maalum ya Ulinzi wa Mtoto ilifundishwa na kundi la wenyeji. Alimkaribisha Esta kuhudhuria. Esta alikwenda siku ya semina, na aliandika mawazo mazuri kwa shauku. Alizungumza tena na mzee Eriki. Akapendekeza ashirikishe mawazo yake kwa Miriam ambaye ni mama mchungaji. Miriam alishauri kwamba kwenye siku ya Watoto duniani kundi la wakina mama liongoze misa nzima na Esta anaweza kushirikisha baadhi ya mambo aliyo jifunza.

Ni mambo gani mazuri yametokea toka Esta aombe?

**Hatua ya 4**

**Kwenye ibada siku ya Watoto duniani, hiki ndicho Esta alicho shirikisha:**

“Watoto ni urithi. Nchi yetu iajengwa na kizazi kipya.

Kama tunavyo tifua ardhi na kulima ili kupa nda mahindi, ni lazima tuandae mazingira salama kwa ajili ya watoto.

Mahindi yanahitaji mvua na mwanga wa jua. Sio mvua nyingi kupita kiasi wala sio jua liwake sana. Watoto wanahitaji kuadabishwa kwa afya na upendo. Ni kama mbegu wasikanywagwe-kanyagwe tu.

Aliwauliza, kanisa la Gloria linapanda vipi mavuno ya Watoto salama?

Alishirikisha jinsi kuna zaidi ya watoto 60 ndani ya kanisa na wengi wa kutoka nje ambao wako tayari na wana shahuku ya kujifunza. Lakini nani atawafundisha?

Alikiri kuwa alichoka na alianza kukata tamaa kuhusu shule ya Jumapili. Alikiri kuwa alipandwa hasira na akatumia tawi pia vikali kwa baadhi ya watoto. Aliwaomba Watoto msamaha.

Mzee Eriki alimwalika Mchungaji tena kurudia wito kwa ajili ya walimu wa shule ya Jumapili.

Miriam alisimama na kusema atawaongoza njia na kukusanya kikundi cha shule ya Jumapili ambao atawafikia yeye binafsi. Alisema, tumekuwa vipofu na viziwi! Sisi tuna wajibika kwa kizazi kipya, kwa nini tunawapuuza hawa watoto ambao Mungu ametupatia?

Mzee Eriki alisema kwamba ameona hitaji kuliweka eneo la kanisa liwe salama na kwamba yeye binafsi atazungushia wigo kuzunguka mashimo ambapo ilikuwa hatari zaidi.

Mchungaji aliliomba kanisa lisimame na kutubu.

- Kulitokea nini kwenye ibada ambayo ilithibitika kuwa njia sahihi ya kuwasiliana na kanisa na kuwashawisi?
- Nani alikuwa na ushawisi hapa?
- Unaona nini hapa ambacho mzizi wake uko ndani ya mtazamo wa kibiblia- ni maandiko gani yanaunga mkono kilicho semwa?